SUPA JACKPOT
TZS. 1,161,795,478
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#


Jumapili Oktoba 15, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581464
www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Serikali** yasema hakuna fidia kwa maafa ya El Nino



UKURASA 3

**Kimiti** asimulia alichotumwa na Nyerere Kilimanjaro

UK. 4



**Mwendokasi** Hiace ulivyoua makada 6 CCM



UKURASA 5

# Dawa kulevya, udumavu vyamshtua Rais Samia

• **Aagiza** hatua zichukuliwe, vinginevyo taifa... *Uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### WAOMBA SIKU YA NYERERE ITENGANISHWE NA MWENGE

PAROKO wa Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria wa Damu Azizi ya Yesu, Butiama mkoani mara, Padre Philip Daniel, na wanafamilia wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, wameiomba serikali ...

UKURASA WA 5



### UHABA WA VIWANDA WAPUNGUZA MAPATO

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, amesema uhaba wa viwanda vya samaki unachangia samaki kusafirishwa nje ya nchi...



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa na viongozi mbalimbali na waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Roho Mtakatifu wakati wa misa maalum ya kumbukizi ya kumwombea Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, iliyofanyika Babati mkoani Manyara jana. **PICHA: UKULU**

## Tanzania kurejesha raia wake walioko Israel

UKURASA 3

## Kutumia VPN bila kibali faini mil. 5/-, jela mwaka mmoja

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA KUSAJILI WATATU WAPYA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM Mkoa wa Morogoro, Dk Rose Rwakatare, akimbeba mmoja wa watoto mwenye ulemavu wa viungo wakati wa ziara yake aliyoifanya katika wilaya mbalimbali mkoani Morogoro wiki hii. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Kasi ya dawa za kulevya, udumavu vyamshtua Samia

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameeleza kushtushwa na kasi ya matumizi ya dawa za kulevya na udumavu miongoni mwa Watanzania unaochangiwa na lishe duni.

Amesema bado kuna tatizo la kilimo cha bangi na uuzwaji wa dawa za kulevya na kuagiza mikoa ambayo bado inalima kilimo hicho kuacha mara moja.

Rais Samia alisema hayo jana katika kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru, ambacho kiliambatana na maadhimisho ya miaka 24 ya Kumbukizi ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliyefariki dunia mwaka 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas, Uingereza alikokuwa akitibiwa.

Maadhimisho hayo na kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru yalifanyika katika Uwanja wa Tanzanite-Kwaraa, Babati, mkoani Manyara, yakitanguliwa na misa maalum ya kitaifa ya kumwombea Baba wa Taifa.

Akizungumza katika sherehe za kilele cha Mbio za Mwenge, kutokana na ongezeko hilo, Rais Samia aliwaagiza wakuu wa mikoa wachukue hatua kali dhidi ya wahusika wanaoendelea kuzalisha dawa hizo na kudhibiti kilimo cha bangi nchini.

**HALI YA LISHE**

Kuhusu hali ya lishe, Rais Samia alisema kwa sasa hairidhishi na kueleza kuwa waathirika wakubwa wamekuwa wajawazito, ambao wana upungufu wa damu kwa asilimia 25, hivyo akawataka wakuu wa mikoa kusimamia mikataba ya lishe katika maeneo yao.

Alisema bado hali ya lishe hairidhishi kwa kuwa wenye uzito uliozidi ni asilimia 32, watoto chini ya miaka mitano wenye udumavu ni asilimia 30 na uzito pungufu ni asilimia 12.

Rais alisema ukondefu ni asilimia tano, uzito uliozidi ni asilimia nne na kiwango cha udumavu kitaifa ni asilimia 30.

Aliitaja mikoa kinara yenye kiwango kikubwa cha udumavu na asilimia kwenye mabano kuwa ni Iringa (56.9), Njombe (54.4), Rukwa (49.8), Kagera (34.3), Simiyu (34.2), Tabora (33.1), Ruvuma (35.6) Manyara ( 32), Songwe (31.9) na Mbeya (31.1).

"Niwaombe sana waheshimiwa wakuu wa mikoa, endeleeni kusimamia mikataba ya lishe, ambayo mlitia mbele yangu," alisema.

**VIRUSI VYA UKIMWI**

Kuhusu kasi ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), Rais Samia alisema watu 54,000 kila mwaka wanapata maambukizi na huku wengine 29,000 kila mwaka wakipoteza maisha.

"Ninaomba kila mmoja ajilinde na awe mlinzi maana ili kudhibiti ugonjwa huu tusibweteke kuwa haupo,"alisema Rais Samia.

Alisema asilimia 96 ya Watanzania wanajua hali zao za VVU na asilimia 97 wanafubaza VVU, hivyo jitihada zinatakiwa kuongezwa na kutaka jamii isibweteke.

**MAKAMU WA RAIS**

Katika misa maalum ya kitaifa ya kumwombea Baba wa Taifa, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akizungumza kwa niaba ya Rais Samia, aliwasihi viongozi na Watanzania kuendelea kumuenzi kwa kuishi katika misingi ya kukemea rushwa.

Pia alitaka wamuenzi kwa kupiga vita umaskini, kutojilimbikizia mali pamoja na kukemea matendo mabaya.

Misa hiyo ambayo pia ilihudhuriwa na Rais Samia, iliongozwa na Askofu wa kanisa Katoliki Jimbo la Mbulu, Anthony Lagwen na ilifanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Roho Mtakatifu, Babati mkoani Manyara.

Dk. Mpango alitoa wito kwa Watanzania kumuenzi Baba wa Taifa kwa kufanya kazi kwa bidii ili kuboresha maisha pamoja na kuinua uchumi wa Taifa.

Alisema ni wajibu kwa Watanzania kumuenzi kwa kuishi maisha aliyoishi Baba wa Taifa kwa kuwa alitumia elimu na vipaji vyake kwa faida ya wote, alithamini dhamana aliyopewa, alikuwa mnyenyekevu na mwenye kujisahihisha alipokosea.

Alisema Baba wa Taifa alikemea matendo mabaya yaliyochochea mmomonyoko wa maadili, alikuwa mwana mazingira hodari na alipiga vita umaskini.

"Serikali itaendelea kushirikiana vema na Kanisa Katoliki pamoja na madhehebu yote ya dini katika kuwatumikia Watanzania. Niwaombe viongozi wa dini muendelee kuliombea taifa amani na utulivu," aliomba.

# Kutumia VPN bila kibali faini mil. 5/- au jela mwaka mmoja

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imepiga marufuku matumizi ya mtandao binafsi (VPN) na kusisitiza kuwa kufanya hivyo ni kosa la kisheria kwa wasio na vibali na atakayebainika adhabu yake ni Sh. milioni tano.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa juzi na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, adhabu ni kiasi hicho cha fedha au kifungo kisichopungua miezi 12 au vyote kwa pamoja.

Alisema katazo hilo ni kwa kuzingatia Kanuni ya 16(2) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui Mtandaoni za mwaka 2020.

"Mtu hatatoa, hatamiliki au hatasambaza teknolojia, programu, programu tumizi au kitu chochote kinachoendana na ambacho kinaruhusu au kumsaidia mtumiaji kupata maudhui yaliyokatazwa.

"Na kwa kuzingatia Kanuni ya 19(b) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui Mtandaoni za mwaka 2020; katika utekelezaji wa majukumu yake ya udhibiti wa maudhui mtandaoni, TCRA ina mamlaka ya kuchukua hatua dhidi ya ukiukaji wa Kanuni ikiwamo kuzuia upatikanaji wa maudhui yaliyokatazwa," alisema.

Dk. Bakari pia alisema kwa kuwa TCRA imebaini upatikanaji wa maudhui yaliyokatazwa kupitia matumizi ya VPN kinyume cha kanuni.

"TCRA inautaarifu umma kwa ujumla, watu binafsi na makampuni ambayo kwa asili ya majukumu na kazi zao, matumizi ya VPN hayazuiliki, kutoa taarifa kwa TCRA juu ya VPN wanazotumia na taarifa zote muhimu ikiwamo anuani ya itifaki ya mtandao (IP Address) kabla ya Oktoba 30, 2023.

"TCRA itaendelea kuchukua hatua za kiudhibiti dhidi ya matumizi ya mtandao binafsi (VPN) yasiyo halali ikiwamo kuzuia upatikanaji wa VPN ambazo hazijatolewa taarifa au kusajiliwa," alisisitiza.

Mkurugenzi huyo alisema TCRA inakumbusha umma kuwa utoaji, umiliki au usambazaji wa teknolojia, programu, programu tumizi au kitu chochote kinachoendana na ambacho kinaruhusu au kumsaidia mtumiaji kupata maudhui yaliyokatazwa ni kosa la jinai.

Alisema ni kosa linaloadhibiwa baada ya kutiwa hatiani, kwa faini ya shilingi za Kitanzania zisizopungua milioni tano au kifungo kisichopungua miezi 12 au vyote kwa pamoja.

**KAULI ACT WAZALENDO**

Wakati TCRA ikitoa angalizo hilo, Chama cha ACT Wazalendo wamepinga vikali taarifa hiyo ya kukataza matumizi ya VPN.

Taarifa iliyotolewa jana na Waziri Kivuli ya Habari na Mawasiliano ACT Wazalendo, Philbert Macheyeki, ilisema vifungu vya kanuni vilivyotajwa ni kandimizi na mwendelezo wa kuzuia wananchi kufurahia haki na uhuru wa kupata habari na kujieleza bila hofu na faragha za watumiaji.

"Tunafahamu VPN zinatumiwa na watu binafsi na taasisi kama benki, mashirika katika shughuli zao za kila siku na kwamba kusalimisha itifaki hizo kwa TCRA kunaweza kurahisisha kuingilia faragha na taarifa binafsi za watumiaji kinyume kabisa na sheria za nchi," alisema.

Aidha, chama hicho kimeishauri serikali kusitisha mara moja kanuni hizo kandamizi na kuacha wananchi, taasisi na mashirika waendelee kuvinjari haki ya faragha, kupata na kutoa habari kama ilivyotolewa na katiba ya nchi.

**HABARI KITAIFA**

# Serikali yasema hakuna fidia El Nino

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

SERIKALI imesema haitalipa fidia kwa mwananchi yeyote atakayeathiriwa na mvua za El Nino na kuwataka wanaoishi maeneo hatarishi wahame kwa ridhaa yao.

Tahadhari hiyo imetolewa wakati Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ikitabiri kuwapo kwa mvua kubwa za El Nino zinazotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Waziri Mkuu, anayesimamia Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura, Prudence Constantine, akizungumza katika maadhimisho ya kimataifa ya kupunguza madhara ya maafa, alisema serikali haina fungu la kulipa fidia wananchi.

Alisema hakuna mtu mwenye uhalali wa kukaa maeneo hatarishi, hivyo hata kama wamekaa muda mrefu, wanatakiwa kuondoka kabla ya mvua hizo kuanza. "Wanaoishi mabondeni au maeneo yote hatarishi, serikali haina fidia ya kuwapa. Tuendelee kuwaelimisha ili waondoke," aliomba.

Constantine aliwataka wakazi hao wasing'ang'anie kusema wana vibali vya kuishi maeneo hayo na wasisubiri kupewa fidia, hivyo ni vizuri waondoke.

Alisema katika idara hiyo ya maafa, hamna fidia ya maisha ya binadamu na yakitokea maafa, kamati elekezi za mikoa, zitaainisha maeneo yaliyoathirika na siyo fidia, bali ni kifuta jasho.

"Ni vizuri wahame mapema kwa kuwa hakuna cha kupewa kiwanja ndiyo wahame, hii tunawapa elimu ya bure na mtu asichukulie poa," alisisitiza.

Alisema katika kukabiliana na maafa ya mvua hizo, timu ya wataalamu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, iko katika mikoa 14, ambayo imetambuliwa na TMA kutoe elimu ya kujikinga na majanga hayo.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni, Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Kigoma, Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Morogoro, Unguja Kusaini, Manyara, Pemba na Unguja Kaskazini. Katika maadhimisho hayo, Mkuu wa Kitengo cha Majanga Asili ya Jiolojia kutoka Taasisi ya Jiolojia ya Utafiti wa Madini Tanzania, Gabriel Mbogoni, alisema athari zinaweza kusababishwa na majanga ya asili ni sunami, vimbunga na tetemeko la ardhi.

Alisema lengo la kuadhimisha siku ya kimataifa ya kupunguza madhara ya maafa kufanyika Oktoba 13 ili kutoa kupunguza majanga ya asili.

Mbogoni alisema wananchi wanaoishi karibu na miinuko waepuke kujenga kwenye miinuko na waendelee kuchukua tahadhali.

Mvua hizo ambazo zimekuwa zikinyesha kila baada ya miaka miwil, kwa mara ya mwisho nchini zilinyesha mwaka 2016 na kusababisha madhara yakiwamo mafuriko.

# Padri, familia waomba Siku ya Nyerere itenganishwe na Mwenge

**Na Vitus Audax,** BUTIAMA

PAROKO wa Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria wa Damu Azizi ya Yesu, Butiama mkoani mara, Padre Philp Daniel, na wanafamilia wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, wameiomba serikali kuheshimu siku ya kumbukizi ya kifo cha mwasisi huyo kwa kuiadhimisha katika siku pekee na kuacha kuiunganisha na matukio.

Siku ya Nyerere ambayo huadhimishwa Oktoba 14 ya kila mwaka, huadhimishwa pia na sherehe za kilele cha Mbio za Mwenge Kitaifa. Kwa mwaka huu, maadhimisho hayo kitaifa yalifanyika Babati, mkoani Manyara.

Padre Daniel alisema hayo jana wakati wa ibada maalumu ya kumwombea Baba wa Taifa baada ya miaka 24 ya kifo chake. Ibada hiyo ilifanyika kanisani hapo na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda.

Alisema suala la kuunganisha tukio la kuzima mwenge kitaifa na kumbukizi ya kifo cha Baba wa Taifa katika maeneo tofauti, inalinyima nguvu tukio hilo na kuwanyima fursa watu wengi kushiriki kikamilifu katika kumbukizi hiyo.

"Taswira ya Baba wa Taifa ni kubwa katika taifa letu na dunia kwa ujumla, hivyo kuunganisha matukio haya kwa sisi wana Butiama hatufurahishwi nalo. Ombi langu kwa serikali siku hizi zitenganishwe,"aliomba.

Pia alisema viongozi wengi na Watanzania wamekuwa wakifika Butiama Oktoba 16 baada ya shughuli za Mwenge lengo likiwa kushiriki katika kumwombea Baba wa Taifa baada ya kukosa nafasi wakati wa siku husika.

"Siku ya Mwalimu ipewe heshima yake kikamilifu kama ulivyo ukubwa wake kitaifa na duniani kwa ujumla. Watu wanahitaji kujua siku hii nini kimefanyika kuhusu Baba wa Taifa kama mzalendo wa taifa hili na mataifa mengine ya Afrika," alisisitiza.

Akizungumza kwa niaba ya familia, kiongozi wa Familia ya Nyerere, Chifu Edward Wanzagi, alisitiza suala la kutenga siku hiyo na matukio mengine kama sehemu ya kuenzi utumishi wake kwa Watanzania.

Chifu Wanzagi aliomba nafasi ya kukutana na Rais wa Samia Suluhu Hassan na wanafamilia kwa ajili ya mazungumzo aliyosema kuwa ni muhimu kwa maslahi mapana ya familia na taifa kwa ujumla.

"Tunaomba tupate siku maalumu tukutane na uongozi wa juu wa taifa tueleze ya moyoni mwetu kama wanafamilia," alisema Wanzagi huku akiwataka

Watanzania kuendelea kuenzi umoja na mshikamano aliouacha Baba wa Taifa katika masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Kuhusu Muungano, Chifu Wanzagi aliwataka wanasiasa kuacha kuubeza bali wakae na kujadili namna sahihi ya kuuimarisha.

Akizungumza kwa niaba ya serikali, Mtanda alisema serikali imeendelea kumuenzi Baba wa Taifa kwa kuboresha miundombinu, kuanzisha taasisi mbalimbali wilayani Butiama lengo likiwa ni kuifanya wilaya hiyo kuwa jicho la taifa.

Aliwataka wananchi wilayani hapa kukazania kilimo na ufugaji hususani katika kipindi hiki cha mvua ili kuiokoa wilaya na baa la njaa linaloweza kujitokeza kutokana na uhaba wa chakula.

Baada ya ibada hiyo, Mtanda aliongoza maandamano ya waumini, wakazi wa Butiama, viongozi wa dini pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali kwenda katika kaburi la Baba wa Taifa kwa ajili ya maombezi.

# Tanzania kurejesha raia walioko nchini Israel

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema imeandaa mpango wa kuwarejesha nchini Watanzania walioko nchini Israel na maeneo mengine ya karibu kutokana na kuendelea kuzorota kwa hali ya usalama.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ilisema imefikia uamuzi huo baada ya kufanya tathmini na kujiridhisha kwamba mazingira ya sasa yanaruhusu kufanyika kwa mchakato huo.

"Kufuatia (kutokana na) kuendelea kuzorota kwa hali ya usalama nchini Israel na maeneo mengine ya jirani, serikali imeandaa mpango wa kuwarejesha nchini Watanzania walioko nchini Israel na maeneo mengine ya karibu," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema Watanzania walio tayari kurejea nyumbani wanashauriwa kujiandikisha kwenye Ubalozi wa Tanzania ulioko Tel Aviv, Israel.

"Wajiandikishe kupitia barua pepe: telaviv@nje.go.tz au simu namna +972 533 044 978 na +972 507 650 , kabla ya Oktoba 15, 2023 saa 6 usiku (yaani leo)," ilisema.

Oktoba 9, mwaka huu, Balozi wa Tanzania nchini Israel, Alex Kallua, alisema hadi siku hiyo ubalozi huo ulikuwa na mawasiliano na Watanzania takribani 350 walioko nchini humo kasoro wawili ambao ni wanafunzi.

"Tumeendelea kuwafuatilia Watanzania wawili ambao ni wanafunzi waliokuwa wanafanya mafunzo kwa vitendo kusini mwa Israeli. Tunafanya jitihada za kuwapata kwanza ili kufahamu waliko na hali zao," alisema Balozi Kallua.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
14.10.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumanne tarehe 17-10-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero, gari hilo lina namba za usajili:

   T 853DXS / T 837DJB

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 22.40
   Upana - mita 5.10
   Kimo - mita 5.10

2. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
14.10.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe 17.10.2023 hadi 24.10.2023 kampuni ya CEVA Interfreight itasafirisha gari yenye mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya Dar Es Salaam kuelekea Mzenga, gari hilo lenye namba za usajili

   NRB97300 / NRB54202 na DS00TG GP / NRB53910

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 28.5
   Upana - mita 5.70
   Kimo - mita 4.80

3. Njia itakayotumika: Bandari ya Dar Es Salaam hadi Mzenga kupitia Barabara ya Mandela, Barabara ya Morogoro gari litasafiri muda wa mchana ( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitoke za.

# Kimiti afichua alichomtuma Nyerere Kilimanjaro

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA sehemu ya kwanza ya mahojiano maalum, mwanasiasa mkongwe, Paul Kimiti, alisimulia Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, alivyonusuru Muungano kuvunjika kutokana na kuibuka kwa kundi la wabunge 55 (G55) kutaka kuundwa kwa serikali ya Tanganyika. Sehemu hii ya pili, anafichua simanzi kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Sokoine, na alichomtuma Nyerere Kilimanjaro...

Mwaka 1984 ulikuwa wa simanzi kubwa kwa taifa la Tanzania kutokana na kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Moringe Sokoine. Kongozi huyo alifariki dunia Aprili 14, mwaka huo, kwa ajali ya gari katika eneo la Wami Dakawa mkoani Morogoro alitokea Dodoma kwenye kikao cha bunge.

Kwa jumla, ni msiba uliotikisa nchi kutokana na kiongozi huyo kujibebea sifa kemkem katika uwajibikaji. Alikuwa hana mzaha na kazi. Waliokuwa karibu naye wanasema alikuwa akitoa maagizo, muda waliokubaliana ni lazima liwe limetekelezwa.

Kuna Naibu Waziri mmoja (jina linahifadhiwa) alipewa maagiza kufanya kazi fulani na alianza kumfuatilia lakini hakuwa ametekeleza. Matokeo yake, alimwambia aliyekuwa Rais wa wakati huo, Mwalimu Julius Nyerere, kama hamfukuzi waziri huyo mzembe, basi anajiuzulu. Nyerere ilibidi amtimue naibu waziri huyo.

Wakati anafariki dunia, Sokoine alikuwa ameongoza vyema vita dhidi ya wahujumu uchumi, wafanyabiashara kwa magendo na walanguzi na wananchi waliokuwa wakisaka bidhaa muhimu 'wa tochi' walimfurahia na kumpenda. Lakini kama wahenga wasemavyo chema hakidumu, ndiyo ilivyotokea kwa Sokoine, ambaye uhai wake ulifikia ukomo akiwa na miaka 46 tu.

**KIMITI AFICHUA**

Mwanasiasa mkongwe, Paul Kimiti, wakati kiongozi huyo anafariki dunia, alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, nafasi aliyoishika tangu mwaka 1982 akiwa chini ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa wakati huo, Cleopa Msuya.

Wakati Sokoine anafariki dunia, Kimiti anasimulia kwamba katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kulikuwa na mawaziri wa nchi watatu ambao ni yeye mwenyewe akishughulikia serikali za mitaa na vyama vya ushirika; Getrude Mongella (Tawala za Mikoa) na Anne Makinda (Sera na Uchumi).



Paul Kimiti

Kimiti anasema wakati wakiwa katika nafasi hizo, vita dhidi ya uhujumu uchumi ilipamba moto kwa kuwa ilikuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu- Sokoine. Kutokana na unyeti wa vita hivyo, anasema iliamriwa kuwa mawaziri wote waliokuwa Ofisi ya Waziri Mkuu wapewe ulinzi.

“Kifo cha Sokoine lilikuwa tukio zito na ambalo kila mtu alishangaa kwani lilitokea wakati wote tulikuwa Bungeni, Dodoma. Tulipopata taarifa hizo na Mwalimu Nyerere akalitangazia taifa, kila mtu alishtuka. Sisi tuliokuwa wasaidizi wake wa karibu kwa kweli ilitusikitisha licha ya kwamba mimi nilifanya naye kazi kwa takriban mwaka mmoja tangu aliporejeshwa katika wadhifa ule,” anasimulia.

Kimiti anasema licha ya kufanya naye kazi kwa muda mfupi, anamsimulia Sokoine kuwa ni mtu alikuwa mchapakazi na walimwona ni mkombozi wao katika kutetea watu wa chini kwa kuwa hakutaka watu kuonewa wala wengine kuwaonea wale wa chini kwa sababu ya nafasi zao.

“Kwa kweli alikuwa tegemeo la Nyerere, alisimamia mambo mengi ya serikali na chini yake tulikuwa na mipango mikubwa ya kutekeleza katika serikali. Lakini kubwa zaidi, alikuwa mcha Mungu.

Alitubana mimi na Mongella kwenda kanisani na alituagiza twende kusali Kanisa (Katoliki) la Mtakatifu Petro na alisema wazi kwamba masomo ya Jumapili tutasoma sisi.

“Sokoine hakujiinua wala kujivuna. Kwa upande wetu alituambia wazi kuwa sisi ni mawaziri ofisini na uraiani ni watu wa kawaida tu. Kupewa ile nafasi ya kusoma masomo kanisani, ilitupa heshima sana mimi na Mongella na watu walifurahi sana,” anasema.

**SABABU KILIMANJARO**

Baada ya kifo cha Sokoine, Mwalimu Nyerere alifanya mabadiliko katika Baraza la Mawaziri kwa kumteua Dk. Salim Ahmed Salim kuwa Waziri Mkuu. Mabadiliko hayo, kwa mujibu wa Kimiti, yalimgusa kwa kuwa hakubaki kwenye baraza bali aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

“Sikujua sababu lakini inawezekana Mwalimu alijua nimeumizwa na kifo cha Sokoine hivyo akaona anitoe pale ili niende sehemu nyingine. Nilikuwa mtu wake (Sokoine) wa karibu na nilimsaidia kwa kiwango kikubwa mimi na wenzangu. Wote tuliokuwa naye tulihuzunishwa sana,” anasema.

Pamoja na kumtoa katika nafasi hiyo na kumteua kuwa mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Kimiti anasema kuna maagizo maalum aliyompatia Nyerere kwenda kuyatekeleza katika wadhifa wake huo mpya.

“Kwa jumla, Mwalimu kila alipokuwa anafanya uteuzi, alikuwa anatoa maagizo maalum kwa mhusika. Kwa kwenda Kilimanjaro, Nyerere alinituma kwamba niende nikawafundishe Wachagga (sehemu kubwa ya wakazi wa mkoa huo) namna ya kulima kwa njia ya kisasa kwa sababu alisema wanalima ovyo. Hiyo ilikuwa kazi ya kwanza kwamba nikaitekeleze. Nadhan alinituma vile kwa kuwa mimi kitaaluma ni mtu wa kilimo,” anabainisha.

Kwa mujibu wa Kimiti, baada ya kufika Kilimanjaro, alikutana na aliyekuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Mkoa, Meja Jenerali Silas Mayunga (sasa ni marehemu, alistaafu akiwa Luteni Jenerali) na wakashirikiana katika kutekeleza agizo hizo ambalo anasema lilileta matokeo chanya.

“Kwa kweli hali niliyoikuta kule baada ya kufika ni kwamba kilimo kilichokuwa kikiendeshwa hakikuwa vile inavyotakiwa. Tulishirikiana na Mayunga kuhakikisha wote wanalima kwa njia ya kisasa. Hata tulipopita barabarani tulikuta mistari imenyooka baada ya kuwapa maelekezo na kuyasimamia.

“Popote tulipofika na kukuta mstari umepinda, tuling'oa mazao hasa mahindi na wahusika tuliwapa mbegu wapande upya,” anasema huku akibainisha kuwa baada ya muda mfupi, agizo hilo lilifanikiwa na kilimo katika mkoa kiliongeza tija.

Mbali na mafanikio hayo, Kimiti anasema jambo lingine alilolifanya katika kilimo ni kuanzishwa kwa miradi miwili ya umwagiliaji ya Lower Moshi Irrigation na Ndungu Irrigation katika wilaya ya Same.

“Miradi hii ilikuwa kwa ajili kuongeza tija katika kilimo kwa kuchochea kilimo cha umwagiliaji na kweli ilileta matokeo chanya. Tuliamua kuweka mkazo katika maeneo haya tofauti ili isionekane tunapendelea upande mmoja,” anasema.

Mbali na miradi hiyo ya umwagiliaji, anasema mkoa uliagiza matrekta madogo 200, maarufu kama Kubota, kwa ajili ya kuongeza kasi katika maendeleo ya kilimo ambayo kwa mujibu wa kiongozi huyo, yalihamasisha vijana kujishughulisha na kilimo.

Pia anasema miradi ya umeme vijijini katika mkoa wa Kilimanjaro ilikuwa ajenda nyingine katika kuchochea uzalishaji hasa viwanda vidogo na vikubwa. Alikaa katika mkoa huo hadi mwaka 1989.

**KAZI MPYA KAGERA**

Baada ya kukaa Kilimanjaro tangu mwaka 1989, Kimiti alihamishwa kwenda Kagera kuwa mkuu wa mkoa.

Kazi kubwa aliyotumwa huko haikuwa tofauti na ile ya Kilimanjaro. Huko alitumwa kwenda kuimarisha zao la kahawa ambalo linazalishwa kwa wingi katika mkoa huo.

Katika kutekeleza wajibu huo, anasema alitumia utaalamu wake wa kilimo kwa kushirikiana na wataalamu wengine. Mafanikio yaliyopatikana, anasema ni pamoja na kuimarisha viwanda vya kukoboa kahawa kikiwamo cha Tanganyika Instant Coffeee, maarufu kama TANICA.

“Jukumu lingine lilikuwa kudumisha ujirani mwema baina ya nchi jirani za Uganda, Rwanda na Burundi ambazo hali ya uhusiano ilikuwa imedorora. Nilimtembelea Rais Yoweri Museveni wa Uganda na kumwonyesha orodha ya askari waliokuwa wametekwa mpakani na akashangaa.

“Ujirani mwema huu tuliufanya pia kwa kuimarisha uhusiano baina ya wilaya zinazopakana kwa sababu licha ya kwamba ziko nchi tofauti, baadhi ya watu wa maeneo hayo ni ndugu. Hili tulifanikiwa kwa kiasi kikubwa,” anasema.

Hata hivyo, anasema jambo kubwa lililomsumbua katika mkoa huo ni kukithiri kwa ujambazi na kwamba lilimnyima usingizi.

“Tulipambana na ujambazi kwa sababu walikuwa wengi. Hawa walininyima usingizi na kila sehemu nilikuwa natembea na ulinzi,” anabainisha.

***-Kesho, nini matokeo ya vita dhidi ya uhujumu uchumi? Fuatilia simulizi zake.***

## HABARI KITAIFA

# Wanataaluma wamuenzi Nyerere kwa machapisho

**Na Romana Mallya**

WANATAALUMA katika kumuenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, wamewasilisha matokeo ya machapisho ya kazi zao za utafiti walizofanya kwa ajili ya maendeleo ya jamii kwa ujumla ambazo zinawekwa katika kitabu.

Lengo la kufanya hivyo ni kufikisha ujumbe kwa haraka katika mataifa mbalimbali kuhusu utafiti huo.

Naibu Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA) anayesimamia Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaaluma, Prof. Richard Kangalawe, aliyasema hayo juzi chuoni hapo kwa niaba ya Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, wakati wa kongamano la pili la kitaifa la kitaaluma la Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Kongamano hilo limebebwa na mada kuu isemayo, "Urithi wa Mwalimu Nyerere Katika Uongozi na Maendeleo ya Jamii na Uchumi katika Kipindi Kipya cha Mapinduzi ya Viwanda."

Akizungumza katika kongamano hilo, Prof. Kangalawe alisema kupitia jukwaa hilo, wanataaluma watawasilisha matokeo ya kazi zao za utafiti katika mada mbalimbali. Alisema hiyo ni namna nzuri wanatalaaluma kushirikiana au kushirikisha matokeo ya utafiti walizofanya kwa ajili ya maendeleo ya jamii kwa ujumla. "Ili kuufikia umma mkubwa wa dunia, mada zinazowasilishwa katika kongamano hili zinachapishwa katika kitabu ambacho kitapatikana kwa wadau mbalimbali lengo ni ili waone matokeo ya utafiti mbalimbali zilizofanyika. Matokeo ya kongamano la mwaka 2022 tayari yapo kwenye kitabu," alisisitiza.

Prof. Kangalawe alisema chuo hicho kinaendelea kumuenzi Baba wa Taifa kupitia makongamano yanayozingatia maono na falsafa zake huku akisisitiza kuwa kongamano hilo ni moja ya namna ya kumuenzi Mwalimu Nyerere katika mada zinazozingatia mambo aliyoelekeza yatekelezwe.

"Makongamano ya aina hii hufanyika mara mbili kwa mwaka. Kongamano la mwezi Aprili ambalo linakumbuka siku ya kuzaliwa kwake na kuanzia mwaka jana kumekuwa na kongamano la mwezi Oktoba tuliona tubadilishe mukhtadha wake kidogo ili liwe la kitaaluma, hivyo mwezi Oktoba tunafanya kongamano la kitaaluma," alisema.

Pia alisema ndani ya chuo moja kati ya mambo ambayo wanayaendeleza ni uwapo wa mafunzo ya uongozi na maadili katika ngazi mbalimbali.

Alisema awali, chuo kilikuwa kinatoa mafunzo ya uongozi kozi fupi za wiki mbili mpaka miezi mitatu na sasa yanatolewa kwa ngazi ya Cheti, Diploma, Shahada ya Kwanza na Shahada ya Umahiri. Mtiva Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii chuoni hapo, Dk. Luzabeth Kitali, katika wasilisho lake lililolenga misingi ya Baba wa Taifa katika falsafa ya siasa ni kilimo alisema limeangalia mchango wa watu wanaohama kutoka mijini kwenda vijijii katika sekta ya kilimo.

"Limeonesha ni kweli watu wanatoka mjini kwenda kijijini na kuna vitu ambavyo wa anavipeleka kama kama zawadi za kifedha na zimesaidia kukuza kilimo kwa wananchi waliopo vijijini kukua kiuchumi na kuongeza kipato," alisema.

Alitaka jamii kuendelea kuziishi siasa za Baba wa Taifa ambazo zinaendelea kuishi na ndio maana watu wanaweka nguvu sekta ya kilimo.

Pia alitoa wito kwa jamii kukisoma kitabu ambacho wanataaluma wametoa mchango wao humo kwa kuwa, kimeibua mambo mbalimbali muhimu kwa taifa ambayo yanakwenda moja kwa moja katika miongozo, misingi na falsafa ya Mwalimu Nyerere.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wanafunzi wa MNMA, Geofrey Malila, alisema kongamano hilo linahamaisha mambo mazuri hususani uzalendo na maendeleo mbalimbali katika nyanja tofauti ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Alisema kila mtu anapaswa kuishi katika imani ya uzalendo ili kuweza kumuenzi Baba wa Taifa.



Kaimu Mkurugenzi wa Utawala Usimamizi na Rasilimali watu kutoka Wizara ya Nishati, Bahati Mtono (kushoto), Makamu Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Sergio Valdaini (kulia), na Mkuu wa Rasilimali asilia kutoka Umoja wa Ulaya, Lamine Dialla, wakivuta kitambaa kuzindua chumba cha programu ya utafiti wa nishati safi ya kupikia katika Taasisi ya Teknolojia DIT jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uhaba viwanda samaki wapunguza mapato

**Na Beatrice Shayo**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, amesema uhaba wa viwanda vya samaki unachangia samaki kusafirishwa nje ya nchi bila kuchakatwa na kupunguza mapato ya taifa.

Mnyeti aliyasema hayo juzi Dar es Salaam alipokuwa akifunga mafunzo ya namna ya kukusanya takwimu za uvuvi katika maziwa makubwa.

"Hatuwezi kusafirisha vichwa vya samaki, ni lazima samaki awe amechakatwa kufikia kwenye matumizi ya mlaji kwa sasa tunahamasisha watu kufungua viwanda,"alisema Mnyeti.

Alisema hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan alifungua bandari ya uvuvi ambao tafsiri yake ni kwamba watasafirisha minofu ambayo iko tayari kwa matumizi na si samaki.

Mnyeti alisema kusafirisha samaki ni hasara ni kama kusafirisha ng'ombe kwenye meli ambapo hiyo haina faida kwa taifa na hata kwa mfugaji.

"Watu wajitokeze kwa wingi kufungua viwanda ambavyo vitasaidia kuchakata kwenye mnyororo wa thamani wa samaki ili tuuze minofu badala ya samaki," alihamaisha.

Mnyeti alisema kwa sasa watafahamu takwimu za viumbe walivyo navyo ndani ya bahari ili kuviendeleza na kuleta mchango kwenye pato la taifa. Alisema sekta hiyo bado ina mchango mdogo katika pato la taifa inachangia asilimia saba na kushuka chini.

"Sekta hii inachangia asilimia saba katika pato la taifa ambao ni ndogo. Ndiyo maana tupo hapa kwenye mafunzo tukishapata takwimu itasaidia kuongeza mchango katika pato la taifa," alisema.

Mkurugenzi wa Utafiti na Uratibu, Dk. Mary Kishe, alisema warsha hiyo imeangalia mambo mawili makubwa kwa namna gani takwimu hizo zinasaidia uendelevu wa rasilimali za uvuvi.

Alisema jambo lingine ni namna ya kuwashirikisha watunga sera na wale wanaosimamia rasilimali za uvuvi kwa kuangalia takwimu zinawapa uhalisia wa mchango wa sekta ya uvuvi kwenye uchumi wa taifa. Ofisa Uvuvi Mkuu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Lilian Ibengwe, alisema kwa siku tano wamejifunza mambo mengi kutoka kwa wataalamu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) na Chuo Kikuu cha Duke ambao watafanya kazi na Taasisi ya Uvuvi Tanzania (TAFIRI).

## Mwendokasi Hiace ulivyoua viongozi, makada sita wa CCM

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

VIONGOZI sita wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamefariki dunia na wengine 12 kujeruhiwa katika ajali iliyotokea juzi jioni katika kijiji cha Ndulamo, Iwawa, wilayani Makete mkoani hapa.

Ajali hiyo imetokea wakati viongozi hao wakitoka katika mkutano wa mlezi wa chama, Mkoa wa Njombe, Halima Mamuya, uliokuwa ukifanyika wilayani humo.

Viongozi waliokufa ni kutoka Kata za Tandala, Lupila na Ipepo wilayani Makete, ambao walikuwa wakisafiri kwa gari T 733 BBP aina ya Toyota Hiace lililokuwa likitoka Makete kwenda Tandala.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, John Imori, alisema ajali hiyo ilitokea saa 11:00 jioni na gari hilo lilikuwa na abiria 18. Alisema lilipofika kwenye kona, lilipinduka na miongoni mwa waliofariki dunia ni wanawake watatu.

"Chanzo cha ajali ni mwendokasi ambao dereva alishindwa kulimudu gari kwenye kona na eneo hilo kulikuwa na mteremko. Majeruhi ni pamoja na dereva wa gari hilo ambao wako katika Hospitali ya Misheni ya Consolata Ikonda na wengine Hospitali ya Wilaya ya Makete," alisema.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Ikonda, Dk. Andrea Mombo, alisema wamepokea majeruhi 11 na mtoto wa miezi tisa.

"Mmoja wa majeruhi hao waliochukuliwa eneo la tukio alifika hospitalini akiwa ameshafariki dunia tayari ambaye ni mama mwenye umri wa miaka 47 kutoka kijiji cha Lupila. Majeruhi wengine akiwamo mtoto, wanaendelea na matibabu.

"Wengi wao wamevunjika miguu na kuna wawili tunataka kuangalia uti wa mgongo kama una shida. Kwa ujumla wanaendelea vizuri na matibabu," alisema Dk. Mombo. Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Dk. Juma Mfanga, alisema tayari timu ya madaktari bingwa wengine kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo, wamefika hospitali ya ya Ikonda kuongeza nguvu.

Katika salamu za rambirambi zilizotolewa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Halima Mamuya, ambaye pia ni mlezi wa chama hicho mkoa wa Njombe, alisema ajali hiyo imekuwa ni pigo kwake.

Alisema imetokea wakati mkutano umekwisha na ameishukuru serikali kwa kuchukua hatua za haraka kuhakikisha majeruhi wote wanapata matibabu.

"Ni jambo gumu kwa sababu tulikuwa tumeshamaliza mkutano na wengine waliopoteza maisha tunawafahamu na tumewasikia wakizungumza. Bila ya shaka zilikuwa kauli zao za mwisho. Kwa hiyo ni jukumu letu sisi kufuata kutekeleza yale ambayo tuliahidi kuyatekeleza,"alisema Halima.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni wakati mwafaka watoa huduma usafiri mwendokasi wakaongezwa

**JIJI** la Dar es Salaam lilikuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ya msongamano wa magari barabarani nyakati za asubuhi na jioni. Hali hii ilisababisha wakazi wengi kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kutokana na kuchelewa kufika kazini na kurejea nyumbani baada ya saa za kazi.

Kutokana na tatizo hilo, serikali ilianzisha mipango mbalimbali ili kuwaondolea shida ya usafiri wananchi hasa ya kukaa muda mrefu barabarani badala ya kuzalisha au kushiriki masuala ya kijamii.

Miongoni mwa mipango hiyo ni kuanzisha usafiri wa treni katikati ya jiji na sehemu za pembezoni, maarufu kama treni ya Mwakyembe. Njia nyingine ni kuongeza barabara shikizi na za pembezoni pamoja na kujenga barabara za mabasi yaendayo kasi, maarufu kama mwendokasi.

Kwa ujumla usafiri huu wa mwendokasi umewasaidia wananchi kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa wakati. Watu wa kutoka Kimara hadi Gerezani, Kivukoni au Kinondoni Morocco, wamekuwa wakipata unafuu wa safari kutokana na kuwapo kwa usafiri huo mzuri. Pia wale wa kutoka Kivukoni au Gerezani hadi Kinondoni Morocco, wamepata unafuu mkubwa sana kuhusu usafiri wa ndani.

Licha ya usafiri huo kuwanufaisha watu wa maeneo hayo, hata wale wa karibu na sehemu hizo na nje kidogo wamekuwa wakitumia kwa kusafiri umbali mfupi na mabasi ya kawaida ya abiria na hatimaye kufika vituo vya mwendokasi na kupata usafiri huo wa uhakika kuwafikisha maeneo mengine kwa haraka zaidi.

Pamoja na kuwapo kwa usafiri huo, hali imekuwa kinyume cha matarajio na ahadi za serikali kwamba Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) jukumu lake kubwa litakuwa mdhibiti wa usafiri huo pamoja na kumiliki miundombinu huku wamiliki wa mabasi na wawekezaji, wakipewa fursa ya kuingiza magari yao katika barabara hizo na kufanya biashara ya usafiri yanye mtazamo wa kihuduma.

Tofauti na matarajio hayo, ni takriban miaka minane sasa tangu kuanza kwa usafiri huo na anayetoa huduma hiyo ni Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) ambalo lilibinafshishwa kwa kampuni binafsi ambayo inaendesha shughuli hiyo kupitia kampuni yake ya UDART. Kuwapo kwa mwendeshaji mmoja kumesababisha ukiritimba na utoaji wa huduma usioridhisha.

Kutokana na hali hiyo, wiki hii imeshuhudiwa adha ya usafiri wa mwendokasi kwa wananchi wa Kimara na maeneo ya jirani baada ya kufika kituo cha Kimara Mwisho na kukosa usafiri huku magari mengi yakiwa yameegeshwa pembeni na mengine kwenye yadi iliyoko eneo la Jangwani.

Hatua hiyo ilisababisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, kuingilia kati na hatimaye kuelezwa kuwa adha hiyo ni kutokana na mabasi 90 yanayomilikiwa na mtua huduma- UDART kuwa mabobu. Kutokana na maelezo hayo, Chalamila alitoa wiki mbili kwa mabasi hayo kuwa barabarani ili kuwaondolea wananchi adha ya usafiri. Kuwapo kwa tatizo hilo kuliwaibua wananchi waliozungumza na vyombo vya habari wakiweka bayana kwamba ili kumaliza tatizo hilo, ni wakati mwafaka sasa kuwapo kampuni zingine zitakazotoa huduma sambamba na UDART badala ya kumwacha mtu mmoja akiendesha huduma.


Wananchi hao wana sababu ya msingi kwani hata serikali ilishatangaza kuwa waendeshaji wengine, awe mmoja au kwa njia ya ubia, wakaribishwe katika kutoa huduma hiyo. Pamoja na kauli hiyo ya serikali kuna hali ya giza imetanda ni kwa nini ni miaka minane mwendeshaji bado ni mmoja tu.

Ikumbukwe kwamba serikali inafanya jitihasa kupanua miundombinu ya usafiri huo ikiwamo kutoka katikati ya jiji hadi Mbagala na mwingine Gongo la Mboto. Kwa hiyo kama mtoa huduma atabaki mmoja ina maana hali itakuwa mbaya zaidi kama washindani wengine hawatajitokeza. Wahenga wanasema dimbwi (kuogelea) limekushinda bahari utaiweza? Msemo huu unasadifu na hali halisi ya sasa kwamba UDART imeshindwa kuendesha eneo dogo tu la usafiri wa mwendokasi. Je, zikija njia za Mbagala na Gongo la Mboto itaweza? Ni wakati mwafaka sasa suala hili la usafiri wa mwendokasi likatazamwa kwa jicho yakinifu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

### Wataalam wa afya wanaojihusisha na ukeketaji wadhibitiwe

**WADAU** wa kupinga vitendo vya ukeketaji kutoka nchi 21 za Afrika, walijichimbia jijini Dar es Salaam, kwa muda wa siku tatu ili kuweka mikakati ambayo itawawezesha kufanikisha kutokomeza vitendo hivyo.

Mkutano huo ulianza Jumatatu na kumalizika Jumatano, huku wadau hao wakiwa na maazimio ya pamoja ambayo watakwenda kuyafanyia kazi katika nchi zao ili kuwa na matokeo chanya.

Kwa leo, nitajikita zaidi katika kile kilichosemwa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akifungua mkutano huo, kuhusu hali ya ukeketaji ilivyo duniani.

Anauelezea umma wa wahudhuriaji kuwa wanawake na wasichana zaidi ya milioni 200 duniani wamekeketwa, lakini anaongeza kuwa zaidi milioni 20 kati ya hao wamekeketwa kupitia kwa wataalam wa afya.

Hatua ya wataalam wa afya kutajwa kuwa wanahusika katika vitendo hivyo vinavyopigwa vita, ni wazi wasipodhibitiwa wanaweza kuifanya vita hiyo kuwa ngumu, hivyo ni vyema wangedhibitiwa.

Ninaamini kupitia utaalam wa mambo ya afya walio nao, jamii inaweza kudhani kuwa kila wanachokifanya ni sahihi, na kujikuta ikingizwa katika mtego huo wa ukeketwaji.

Kimsingi wanapotajwa wataalam wa afya, maana yake wanaweza kuwa ni madaktari, wauguzi na watu wengine wa kada hiyo, ambao kupitia taaluma yao wanaaminika katika jamii.

Kwa mantiki hiyo, wanaweza kusababisha vitendo vya ukeketaji vikaendelea kuwapo katika jamii na kuwafanya wadau wanaopambana kutokomeza ukeketaji kuwa na wakati mgumu.

Ikumbukwe kuwa wataalam wa afya ndio hao ambao huwa wanaiambia jamii kuwa ukeketaji ni ukiukaji wa haki za binadamu, unaathiri afya kimwili na kiakili kwa mamilioni ya wasichana na wanawake.

Kwamba waathirika wa ukeketaji wanakabiliwa na hatari katika afya yao na uzima, ikiwa ni pamoja na athari pindi tu baada ya kukeketwa ikiwawamo maambukizi, kuvuja damu nyingi au kiwewe na magonjwa ya muda mrefu ambayo huenda yakatokea maishani.

Vilevile, wanaeleza kuwa wanawake waliokeketwa wana uwezekano mkubwa wa kupata tishio la kupoteza maisha wakati wa kujifungua, kukabiliwa na magonjwa ya akili na maambukizi ya muda mrefu.

Wakati wakieleza madhara hayo, lakini upande pili wapo baadhi yao wanaotajwa kujihusisha na ukeketaji na hivyo kuwapo kwa uwezekano wa vita dhidi ya ukeketaji kuwa na changamoto.

Kwa kuwa ukeketaji unatambulika kama ukiukaji wa haki za binadamu na hauna faida zozote za kiafya na unasababisha madahra, basi ni vyema hao madaktari wakasakwa na kuchukuliwa hatua.

Waziri wameeleza kwa ujumla ni kwamba wanawake na wasichana zaidi ya milioni 20 duniani wamefanyiwa vitendo hivyo kupitia kwa wataalam wa afya, inawezakana wakawamo watalaam wa afya wa Tanzania.

Hivyo zingefanyika jitihada za kuwabaini wataalam wa aina hiyo na kuwachukulia hatua za kisheria, ili kutokomeza vitendo hivyo ambavyo watalaam wenyewe wanakiiri kwamba vina madhaara kiafya.

Kwa Tanzania, mikoa ambayo inatajwa kuwa na viwango vikubwa vya ukeketaji ni Manyara asilimia 58, Dodoma asilimia 47, Arusha asilimia 41, Mara asilimia 32 na a Singida 31.

Hiyo ni kwa mujibu wa utafiti wa Kidemografia na Afya Tanzania uliofanyika mwaka 2015/16 uliobaini viwango hivyo vya ukeketaji nchini, ambavyo huenda baadhi ya wataalam wa afya wanahusika.

Ni kweli kama anavyosema waziri kwamba ukeketaji ni kitendo kinachoondoa utu wa wanawake na watoto wa kike, kuhatarisha afya zao na maisha ya baadaye, hivyo hautakiwi kupewa nafasi katika jamii.

Ingekuwa vyema iwapo viongozi wote kuanzia ngazi ya chini wakiwamo wa dini, mila na asasi za kiraia wangehusika na katika vita hiyo kwa kutoa elimu sahihi na hata kuwataja wote wanaokwamisha mipambano ya kutokomeza ukeketaji ndani ya jamii.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# Hongera Rais Samia kwa shahada ya heshima



**Pascal Mayalla**

KWANZA, nijiunge na Watanzania wengine kumpongeza Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa ziara yake ya kiserikali nchini India. Pongezi zangu za kwanza ni kwenda kwa ndege yetu ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kwani hakuna kitu kinakuza utalii kama uwapo wa ndege ya moja kwa moja, hivyo kitendo cha dege letu kutua viwanja vikubwa vya kimataifa ni sifa na heshima kubwa kwa nchi yetu.

Napongeza sana hili kwa sababu ni moja ya mada zangu za nyuma, yenye kichwa cha habari, "Kwa nini Rais Wetu Anaposafiri Nje ya Nchi, Apande Ndege za Wengine, Wakati Sisi Ndege hizo tunazo na uwezo huo tunao?"

Katika mada hiyo nilishauri gharama isiwe hoja bali aandamane na ujumbe wa wafanyabiashara watakaojilipia. Hili limefanyika, hongera sana.

La tatu ni lile nililoliibua kwenye ule mkutano wa Rais na vyombo vya habari wa mwaka 2016.

Pia nilishauri Rais wetu anapofanya ziara za kitaifa nje ya nchi, aandamane na waandishi wa habari kutoka vyombo vya serikali na vya binafsi na pia tuko waandishi wa kujitegemea wenye uwezo wa kujilipia, hivyo tushirikishwe.

Ziara hii ya India vyombo vyetu vya habari vimeshirikishwa kikamilifu. Hongera sana Zuhura Yunus.

Mada ya leo ni kuhusu shahada za heshima (honoris causa) ambayo ametunukiwa Rais wetu.

Hapa swali la kujiuliza ni je, mtunukiwa anapaswa kuitwa Daktari na kuandikwa Daktari?.

Hapa pia nimpongeze Rais Samia kutunukiwa shahada ya pili ya heshima ya udaktari moja aliyotunukiwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na nyingine katika moja ya vyuo vikuu vya India vyenye heshima kubwa duniani.

Japo marais waliotangulia, Mwalimu Julius Nyerere, Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa walitunukiwa shahada za udaktari wa heshima (honoris causa), hawakuitwa kwa vishangilio vya udaktari, Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete na Rais Samia baada ya kutunukiwa wameitwa madaktari na hata kuandikwa na hadi sasa vyombo vya habari vinawaita hivyo.

Juzi tena nchini India, Rais Samia kaheshimishwa tena kwa shahada nyingine ya heshima ya udaktari wa falsafa. Hakuna ubishi anastahili kutokana na kazi yake nzuri anayoifanya kwa Watanzania katika kuwaletea maendeleo.

Pamoja na kustahili shahada hiyo kwa watu mbalimbali, kiukweli shahada za heshima, hazibadili jambo na kumfanya mtu aitwe kwa kishangilio cha daktari.

Nyerere alipewa lakini hakuitwa na Mwinyi vilevile. Mkapa na mke wake nao walitunukiwa lakini walitoa taarifa kwa umma kwamba wasiitwe kwa kishangilio hicho.

Ili kuondoa mikanganyiko ya nani anastahili kuitwa daktari, kama vile wa binadamu na wanyama pamoja na wale wa shahada za uzamivu (PhD), ni vyema Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ikafafanua hili. Sina kinyongo na shahada za heshima za viongozi hao, zikiwamo za Rais Samia na wengine walizotunukiwa kwa sababu ya kazi walizozifanya kwenye jamii, lakini msimamo uwapo wa nani anastahili kuitwa kwa kishangilio cha udaktari. TCU ilifafanue hili kwa kuzingatia hoja ya Prof. Joseph Kironde.

Naomba kwanza tutofautishe mtu kujiita daktari au profesa. Tanzania tulikuwa na tumeendelea kuwa na watu wanaotambulishwa kwa vishangilio hivyo huku baadhi ikihojiwa wamestahili vipi kuitwa hivyo tena kwa kazi gani? Miongoni mwa watu waliowahi kuitwa hivyo ni Profesa Matikisa, Profesa Singira, Profesa Maji Marefu, Dk. Manyaunyau, Dk. Ngwizukulu Jilala, Dk. Mwaka na Profesa Matunge.

Pia wako walioitwa Rais wa Sinza, Rais wa Wasafi, Rais wa Manzese, hata klabu zetu za mpira na vyama vya michezo navyo vikawa na marais.

Kwa ujumla si vibaya kuitwa lakini ukweli unabaki kwamba unapoandika jina lako kwenye usajili wowote, rasmi, lazima utatumia majina rasmi na kishangilio halisia.

Rais mstaafu wa Marekani, Barack Obama, ametunukiwa shahada za udaktari wa heshima 14 lakini huwezi kusikia popote akiitwa daktari au kuandikwa kwa kishangilio hicho. Kwa vile huu utaratibu wa shahada za heshima, si utaratibu wetu wa jadi zetu, viongozi wetu wanapotunukiwa, ni vyema tukaufuata utaratibu na utamaduni wa shahada hizo.

Wananchi, rukhsa kumwita mtu daktari na kwenye mikutano ya kawaida. Kubwa zaidi, hili linahitaji ufafanuzi wa TCU na baada ya TCU kama ilivyofafanuliwa na Prof. Kironde kwenye jarida la TCU, kuna haja kwa TCU kulitolea ufafanuzi.

Baada ya TCU kulifafanua, MCT nayo ilitolee muongozo kwa vyombo vya habari kuhusu kuwataja au kuwaandika madaktari hawa wa heshima kwa vishangilio vyao vya udaktari.

La mwisho, ni kwa madaktari wenyewe. Nakumbuka kwenye moja ya matukio yaliyokuwa yakitangazwa mubashara na vituo vyetu vya televisheni, mmoja wa viongozi aliteleza ulimi na kumwita Mkuu "Mheshimiwa Mungu" mbele ya mkuu mwenyewe.

Kwenye hili la kuitana kwa vishangilio vya udaktari wa heshima na kukaa kimya, tafsiri yake ni ama wanapuuza, wanaridhia au wanafurahia.

Kwa sababu si wao wanaojiita madaktari na maadam ni kishangilio cha heshima, kuna ubaya gani mtu kuheshimika na kuitwa kwa sifa ya heshima ya usomi ubobezi na ubobevu ili hali ni heshima tu? Je,tuwashauri viongozi wetu wakemee?

Kutokana na maendeleo ya utandawazi, kumeibuka vyuo vikuu vya mtandaoni, vinavyouza shahada bila hata kuingia darasani.

Vyuo vikuu hivi vya mtandaoni vinatoa shahada za udaktari wa falsafa kwa kulipia tu. Jambo hili lisipotolewa mwongozo na ufafanuzi, utafikia wakati tutashindwa kutofautisha yupi ni daktari wa kweli wa kusomea, daktari wa heshima na daktari wa kununua makaratasi. Kwa kufanya hivyo, hakutakuja kuichanganya bure jamii yetu huko mbele ya safari?.

**Wasalaam**

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# Kama tunaongeza makalio acheni tukeketane tu!



**Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)**

UKISTAAJABU ya Musa utayaona ya Firauni." Ni usemi maarufu sana katika lugha ya Kiswahili unaohadharisha watu kwamba unaweza kudhani hili ni la ajabu lakini kumbe liko la ajabu zaidi ya hilo.

Kinachoendelea hivi sasa nchini kinasadifu hali hiyo kwamba tumekuwa tukishangaa mengi yanayoendelea katika taifa hili kumbe yapo ya kustaajabisha zaidi yanayozaliwa na kuibuka kila kukicha.

Kwa siku nyingi tu nchini, kumekuwa na vita vikiendelea dhidi ya mila zinazoitwa potofu miongoni mwa makabila nchini; mila ya ukeketaji inayodaiwa kudhalilisha utu wa mwanamke.

Yako makabila ambayo yamekuwa yakiamini kwamba mwanamke anayekeketwa ndiye anayetakiwa na jamii kwa sababu kufanya hivyo humweka katika adabu na kuondokana na macho juu au ukahaba.

Mabilioni ya fedha yamekuwa yakitumiwa na serikali lakini pia na asasi za kiraia kutoa elimu kwa jamii dhidi ya tabia hiyo, huku mangariba wakipigwa vita na hata baadhi yao kufikishwa mahakamani.

Watoto wa kike katika makabila hayo, wamekuwa wakielimishwa na kuhadharishwa kuwa ni njia potofu wanayofanyiwa katika kinachodaiwa ni kutaka kuwajengea tabia njema na hatimaye kuwa wake bora wenye maadili mema kwa familia na jamii kwa ujumla.

Ukeketaji ni kitendo cha kuondoa sehemu ya siri ya mwanamke kama inavyofanywa tohara kwa mwanamume, ingawa kwa mwanamume inaungwa mkono, kwa mwanamke inaonekana dosari.

Lakini mara nyingi matatizo ya kiafya yamekuwa yakitumiwa kukabiliana na kitendo hicho, wakeketwaji wakitishiwa kuwa kufanyika kwa kitendo hicho kunaweza kuathiri tendo la ndoa lakini pia uzazi.

Wanaozingatia elimu hiyo, wamekuwa wakikwepa kukeketwa na hata mangariba wakikimbia kukeketa watoto wa kike na katika baadhi ya jamii, kitendo hicho kinaonekana kuwa ushamba kama si ujima na kupigwa vita ili kukoma kabisa.

Inawezekana wahenga walipoanzisha utaratibu huo kwa wanaume na wanawake, walikuwa na kusudi lao kwa jamii na kubwa likiwa ni adabu, heshima na nidhamu, lakini vizazi vya leo vikabaini kuwa kwa mtoto wa kike si sawa.

Hapana uthibitisho wa dhahiri wa kiafya kwa wakeketwao, zaidi ya kutokwa damu nyingi lakini bila kusababisha ulemavu wa kudumu, kwani hata waliofanyiwa hivyo huzaa na kupata na kujenga familia zao kama wasiokeketwa.

Lakini wakati huu ambao vita dhidi ya ukeketaji vikiendelea, sasa kumeibuka utamaduni mpya miongoni mwa binadamu, wa kujikataa kimaumbile na kumkosoa Muumba na kutaka sasa kujiumba wenyewe.

Watu sasa wanakataa unene, wembamba, weusi na kutaka kuonekana tofauti na walivyozaliwa, huku wakisahau kuwa huzaliwa kwa mfano wa wazazi wao kama ambavyo Mungu alituumba kwa mfano wake.

Watu wanaona kope walizopewa haziwatoshi, wanataka nyingine nyingi na ndefu, kucha haziwatoshi wanataka ndefu zaidi, rangi haiwatoshi wanajichubua, nywele haziwatoshi wanavaa za bandia.

Kana kwamba haitoshi, makalio hayawatoshi wanataka makubwa zaidi, matiti ni madogo wanataka mizigo mikubwa, matumbo makubwa hawayataki wanataka madogo, mikono wanataka myembamba, hivyo sasa hospitali zimepata kazi ya kuwabadili.

Juzi kati hapa tukatangaziwa kuwa hospitali kubwa nchini itaanza kubadili makalio ya wanawake kwa kuyaongeza ukubwa, matiti kuyajaza zaidi. Hiyo inakuja siku chache baada sangoma wa Kanda ya Ziwa kutaka kuwakuza matiti mabinti pacha na matokeo yake wakapoteza maisha!

Inaonekana mpaka tunawekewa bei elekezi ya upasuaji huo, ina maana umehalalishwa na sasa mamilioni ya fedha yatatumika kutengeneza watu 'maroboti' kwa nia tu ya kufurahishana kimapenzi! Watanzania na Serikali yetu sijui nani katuroga?

Tunakataa nini na tunataka nini? Tumestaajabu ya Musa na kwa kweli sasa tunaona ya Firauni? Tunapniga ukeketaji tukiaminhishwa madhara yake lakini tunaunga mkono upasuaji makalio na kuyaongeza ukubwa tukijua fika madhara yake? Tunataka kumfurahisha nani?

Kweli tumeagiza mitambo na kuiingiza nchini kwa mabilioni ya fedha kuja kupasua makalio na matiti ya wanawake eti kufurahisha wapenzi na wapenda ngono kweli? Viongozi wa nchi hii ndivyo mlivyojipangia kulipeleka taifa?

Hii ni sawa na kuzuia na kukataza matumizi ya bangi, mirungi na mihadarati mingine, huku tukiruhusu uvutaji shisha! Mangariba wa Kitunda wasikekete, lakini mashangingi wa Buza waongeze ukubwa wa makalio na matiti tena katika hospitali inayoheshimika nchini. Safari ni ndefu sana na tutafika tumechoka Watanzania. **Tuombeane!**

# Mradi elimu ya juu kuongeza wataalamu

**Na Miraji Msala**

Mradi wa Mageuzi ya Kiuchumi kupitia Elimu ya Juu (HEET) umekusudia kusaidia nchi kuongeza watalamu wa sayansi katika kipindi kifupi kijacho.

Hayo yamesemwa juzi na Mkurugenzi wa Elimu ya Juu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Kennedy Hosea, wakati akizindua programu maalumu ya msingi kwa wasichana inayofadhiliwa na HEET, Kinondoni mkoani Dar es Salaam. Dk. Hosea alimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Caroline Nombo.

"Tunataka tuongeze idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu nchini. Wanaojiunga elimu ya chuo kikuu nchini kwa sasa ni asilimia saba pekee, sasa tunataka tupandishe hiki kiwango. Huu mradi wa HEET utasaidia kupata wanafunzi ambao hawapo katika mfumo rasmi kwa lengo la kuwawezesha kupata sifa na kuongeza idadi ya wanaojiunga na elimu ya juu nchini na tunatarajia kupata wataalamu kutoka kwenye kundi hili siku zijazo," alisema Dk. Hosea.

Aidha, Dk. Hosea aliwataka wanafunzi waliopata fursa hiyo kujiandaa vyema ili kufikia malengo yao ambayo awali yalififishwa kutokana na changamoto mbalimbali zilizowakabili. Aliwataka pia wawe mfano kwa kufanya vyema ili kuipa nguvu serikali na hatimaye kuongeza udahili na ufadhili wa namna hii kwa wasichana wengine wenye uhitaji kutoka jamii ambazo hazijafaidika sana na elimu ya juu. Mkurugenzi huyo aliishukuru serikali hasa Rais Samia Suluhu Hassan kwa maono yake yenye mawanda mapana katika kuwaletea maendeleo Watanzania katika nyanja zote na elimu ikipewa nafasi ya juu kabisa.

"Haya yote yanayofanyika katika sekta ya elimu ni maelekezo kutoka kwa Rais wetu. Mara tu alipoapa kuwa Rais, aliagiza kufanya mapitio ya mitaala, sera na Sheria ya Elimu nchini na kwa sasa wizara imefika hatua ya juu katika kutekeleza maelekezo hayo. Tunasubiri vyombo vya uamuzi vijadili na kuridhia ili utekelezaji uanze. Mabadiliko hayo yanalenga katika kuzalisha wahitimu wenye elimu ujuzi ambao wataweza kujiajiri na kuajiri wenzao," aliongeza.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Prof. Elifas Bisanda, aliishukuru Benki ya Dunia kwa kushiriki kwa kiwango kikubwa katika kuchangia maendeleo ya chuo hicho tangu kuanzishwa kwake. Kwa sasa benki hiyo imefadhili wanafunzi 1,000 na alihakikishia benki hiyo pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuwa chuo kimejiandaa vyema kuendesha mafunzo hayo.

Awali akitoa maelezo ya utambulisho wa programu maalumu ya msingi kwa wanafunzi wa kike katika ufunguzi huo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Taaluma, Utafiti na Huduma za Ushauri wa Kitaalamu, ambaye pia ndiye mratibu wa mradi wa HEET chuoni, Prof. Deus Ngaruko, alisema OUT imejiandaa kutangaza awamu ya pili ya udahili kwa wanafunzi wa programu hiyo ambao wataanza kusoma Desemba, mwaka huu, ikiwa ni mchakato wakufikia malengo yaliyopangwa na mradi.

Mradi wa HEET umetoa ufadhili wa wanafunzi 1,000 kwa kipindi cha miaka mitano kwa wanafunzi kusoma progam maalumu ya msingi katika masomo ya sayansi kwa wasichana waliokuwa wamekosa sifa za kujiunga moja kwa moja vyuo vikuu katika ngazi ya shahada za kwanza.

Wanfunzi wa kike wapatao 140 wamejiunga na mafunzo katika awamu ya kwanza na watakaofanikiwa kumaliza vyema watajiunga na elimu ya juu katika vyuo mbalimbali nchini na wanatarajiwa kunufaika na mikopo itolewayo na taasisi mbalimbali za mikopo nchini.

# Bil. 713/- zatolewa kukuza ushiriki wananchi kiuchumi

**Na Romana Mallya**

SERIKALI kupitia mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 713.8 ili kukuza ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi.

Mikopo hiyo imetolewa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo juzi Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mwanamke Anayeishi Kijijini ambayo kila mwaka hufanyika Oktoba 15.

Alisema kwa mwaka huu, maadhimisho hayo yanatarajiwa kufanyika leo katika Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, ikiwa ni utekelezaji wa Azimio la Umoja wa Mataifa Namba 62 lililopitishwa Desemba 18, 2007.

"Tanzania itaungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku hii muhimu ambayo hapa nchini ilianza kuadhimishwa mara ya kwanza mwaka 2018 ikiwa na lengo la kutambua jitihada na mchango wa wanawake wanaoishi vijijini kwa maendeleo ya jamii," alisema.

Waziri Gwajima alisema mikopo iliyotolewa imezalisha jumla ya ajira 3,122,104, kati ya ajira hizo, wanawake ni 1,623,494 sawa na asilimia 52 na wanaume ni 1,498,610 sawa na asilimia 48.

Alisema mikopo hiyo imetolewa kwa wajasiriamali 2,203,838 na kati yao, wanawake ni 1,234,149 sawa na asilimia 56 na wanaume 969,689 sawa na asilimia 44, katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwamo sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Vilevile, alisema serikali imewezesha kutungwa kwa Sheria ya Ardhi ya Kijiji Namba 5 (1999), Kifungu cha 20(1), ambacho kinatoa nafasi kwa wanawake kumiliki ardhi.

"Hatua hiyo imeleta matokeo ya ongezeko la umiliki wa ardhi kwa wanawake ambapo upatikanaji na umiliki wa ardhi kwa wanawake umeongezeka ambapo hadi kufikia 2021/22, jumla ya Hatimiliki za Kimila 1,171,884 zimetolewa kwa wanawake 406,915 na wanaume 764,969. Hatimiliki 916,765 zilitolewa kwa wanawake 228,203 na wanaume 688,562," alibainisha.

Pia alisema serikali katika jitihada za kumwezesha mwanamke kiuchumi na kumuongezea muda wa uzalishaji mali, imemarisha huduma ya upatikanaji maji vijijini chini ya kampeni ya "Mtue Mama Ndoo Kichwani" ambapo upatikanaji maji ni asilimia 77 na lengo ni kufikia asilimia 85.

Alisema hiyo imewezesha kumpunguzia mzigo mwanamke wa kutafuta huduma ya maji sambamba na kumwezesha kuwa na muda wa kushiriki shughuli za kiuchumi

Kuhusu maadhimisho hayo, Dk. Gwajima alisema lengo kuu ni kutambua na kuuenzi mchango wa wanawake wanaoishi vijijini hususan katika nyanja za uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuhakikisha usalama wa chakula cha kaya na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa.

Waziri huyo alitaja malengo mengine kuwa ni pamoja na kuongeza mwitikio wa wanawake kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kushiriki katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Kadhalika alisema kujenga uelewa kuhusu fursa za uwezeshaji wa wanawake kiuchumi; kuhamasisha wanawake fursa za kibiashara na matumizi ya zana na Teknolojia sahihi na rahisi za uzalishaji zinazorahisisha kazi ili kuweza kumudu ushindani wa kibiashara sokoni.

Alitaja nyingine ni kutoa hamasa kwa wanawake wa jamii kuhusu kukabiliana na umaskini wa kipato, ambao ni nguzo muhimu ya uhakika wa chakula, lishe na malezi katika kaya.

Alisema kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inasema, "Wezesha Wanawake Wanaoishi Kijijini: Kwa Uhakika wa Chakula, Lishe na Uendelevu wa Familia".



Wananchi wakiwa wakishuhudia ajali aliyotokana kugongana kwa gari dogo na Pikipiki katika eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni pikipiki iliyogongwa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwenyekiti Wazazi ataka miradi ya kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Morogoro, Dk Rose Rwakatare, amehitimisha ziara yake mkoani humo akiwataka viongozi kuanzisha miradi ya kiuchumi ya jumuiya.

Dk. Rwakatare alitembelea wilaya za Malinyi, Kilombero, Ulanga, Kilosa, Mvomero, Gairo, Morogoro Mjini na Morogoro Vijijini.

Akizungumza wakati akihitimisha ziara hiyo juzi mjini Morogoro, Dk. Rose aliwaasa wazazi kusimamia maadili mema katika jamii na kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia na matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema kila wilaya iwe na nyumba za watumishi wa jumuiya hiyo na kusisitiza umoja na mshikamano ndani ya jumuiya.

Mwenyekiti huyo alitembelea watu wenye mahitaji maalum kuwafariji kwa kuwapa baadhi ya mahitaji mbalimbali na kuiasa jamii kujenga utamaduni wa kutembelea familia zenye mahitaji na kutoa msaada wa vitu mbalimbali .

Dk. Rwakatare alisisitiza uhai wa chama na Jumuiya ya Wazazi na alikagua miradi mbalimbali ya jumuiya na serikali huku akisisitiza viongozi kujitahidi kutatua baadhi ya changamoto zinaikabili jumuiya hiyo .

Mwenyekiti huyo pia alikagua miradi ya ufugaji wa kuku na ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Gairo na wilaya kilombero na kuahidi kuwa atasaidia ujenzi wa nyumba hizo.

Pia aliahidi kuchangia mifuko ya saruji katika ujenzi wa zahanati ya Ipopoo na kuwapatia taulo za kike wanafunzi wa ya sekondari Miembeni Wilaya ya Malinyi.

Katika ziara hiyo, Dk Rwakatare alikagua mradi wa shamba la mikorosho na kuchangia pesa kwaajili yakununua kiwanja cha ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa CCM Wilaya ya Morogoro Mjini na kutembelea mradi wa ujenzi wa bwawa la kufugia samaki.

Kutokana na changamoto ya usajili wa wanachama wapya wa Jumiya ya Wazazi Mkoa wa Morogoro, Dk. Rwakatare aliwakakadhi kadi 500 za jumuiya kwa kila wilaya na kuwataka viongozi katika wilaya hizo kuongeza idadi ya wanachama wasiopungua 100 kwa mwezi.

Aidha, alihamasisha umuhimu wa michezo kwa kutoa vifaa ya michezo wilaya zote alizotembelea ikiwemo jezi na mipira ya miguu ili wawezekuanzisha ligi katika wilaya zao na kutumia fursa hiyo kupata wanachama wapya wa jumuiya ya wazazi.

# MAISHA

OKTOBA 15, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14




## Pika Katles ufurahie maisha

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15






## KATUNIKA


Ukurasa 16



# FURAHIA 'SWEATPANTS' Hustarehesha kwenye mazoezi

Ukurasa 13


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | ■ | M | B | U | G | A |
| H | ■ | ■ | ■ | G | ■ | N |
| A | ■ | D | A | U | ■ | Z |
| B | E | I | ■ | M | E | I |
| A | ■ | M | B | U | ■ | S |
| H | ■ | B | ■ | ■ | ■ | H |
| A | M | A | N | A | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


TIN, WAO, NAE, KWA, SHIBA, IMANI, IKATE, KONDA, BWAWANI, AMINIKA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

HAYA WATOTO WAZURI, TUTAFUTE NJIA YA KWENDA NYUMBANI KUANZIA HERUFI A MPAKA B.




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO wa miaka sita alimuuliza babake:

MTOTO: Baba, eti sisi wanadamu tulikuja vipi duniani?

BABA: Mungu alimuumba Nabii Adam na Hawa. Kisha wao wakaanza kuzaa watoto na watoto wakazaa mpaka tukazaliwa sisi. (Mtoto hakuridhika akamfuata mamake)

MTOTO: Mama, eti sisi wanadamu tulikuja vipi duniani?

MAMA: Wanasayansi wamesema sisi tulitokana na manyani baadae tukawa binadamu. (Mtoto akarudi kwa baba)

MTOTO: Baba mbona mama anasema sisi tulikuwa manyani mwanzo?Au wanidanganya?

BABA: Mwanangu, mimi nimekuelezea kuhusu ukoo wetu. Mamako amekuelezea kuhusu ukoo wao.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mume, mke washindana kuzaa nje ya ndoa!

KARIBU tena msomaji wangu. Wiki iliyopita mada ilihusu "Mimba ya nje, anakunywa sumu, kisa mume kaoa mke mwingine".

Ni kisa cha msomaji wa safu hii alinisimulia kupitia ujumbe wa simu ya kiganjani, inaelezwa baada ya kuigida sumu ya panya, majirani walimnusuru kwa kumkimbiza hospitalini.

Msomaji wetu huyu, hata hivyo, aliahidi kumdadisi mama huyo aliyetaka kujiua kujua nini hasa kilichomfanya achukue uamuzi ule, jambo ambalo alilifanya na yafuatayo ndiyo yaliyojitokeza;-

"Anti, nilimuuliza yule mke mnywa sumu sababu akaniambia kuwa hakuwa ameimeza bali aliiweka kinywani akijaribu kumtishia mumewe.

"Nilijaribu kuchimbua kwa undani kwa kushirikiana na majirani kuhusu tukio lile, nikabaini mambo mengi mno katika ndoa yao. Sehemu kubwa kati yao ni kwamba uaminifu hakuna.

"Mifano hai ni kuwa mtoto wa pili siyo wa mumewe na huyu mama alikuwa na bwana nje, wakati huo huo mumewe naye alikuwa na mwanamke nje mwenye mtoto wa kiume.

"Nikagundua kuwa huyu mke amezoea haoni vibaya kubeba mimba za nje ya ndoa za mabwana tofauti tofauti na hadi sasa ana watoto wanne kati yao, wawili siyo wa mumewe hata sura zao ni tofauti.

"Naye mumewe siyo mtulivu kwani huyu mke wa pili aliyemuoa siyo yule aliyezaa naye. Nadhani mambo yanafichika kwa kuwa huyu bwana wa sasa huwa anakuja kwa msimu kwani naye ana mke huko kwao. Ndio maana akachukua picha za yule mtoto akawaonyeshe ndugu zake kwao."

Katika kisa hiki ambacho ni mwendelezo wa wiki iliyopita, liko tatizo kubwa kwa kinababa wengi kubambikizwa watoto. Iko ripoti moja iliwahi kutolewa na ofisi ya uchunguzi ikionyesha kuwa zaidi ya asilimia 48 ya wanaume waliojitokeza kupima vipimo vya vinasaba (DNA), waligundulika kubambikiwa watoto. Ni utafiti ndani ya miaka mitatu.

Ripoti ikaenda zaidi kwamba asilimia 48.32 ya watoto waliofanyiwa vipimo vya DNA kwa kipindi hicho, waligundulika hawalelewi na baba halali.

Naam. Kinababa mpo? Haya, tafakari kwa makini kisa hicho hapo juu na jinsi familia hiyo inavyofanyiana mzaha katika maisha. Mke aliyejaribu kunywa sumu kwa kumtishia nyau mumewe, kumbe naye watoto wawili kati ya wanne wamepatikana nje ya ndoa.

Mumewe naye mke aliyemwoa wala siye yule aliyezaa naye mtoto nje ya ndoa. Kwa ujumla, viongozi wa kaya hii wote wanafanyiana mzaha kila mmoja akionyesha ubabe wa kuwa na mahusiano nje ya ndoa.

Sasa katika hali kama hiyo nani wa kumnyooshea kidole mwenzake? Uaminifu umetoweka ndani ya nyumba nyingi na matokeo yake kila mmoja anafanya vile atakavyo na wala hakuna anayeonyesha kujali. Je, ni familia gani hii?

Baba, kama ilivyo sheria za dini yake anaruhusiwa kuoa mwanamke zaidi ya mmoja. Lakini je, huyu bi mkubwa, mume huyu kwanini hafuatilii nyendo zake?

Kama ana mahusiano nje ya ndoa na ana wanaume tofauti kama ambavyo watoto wanaonyesha sura tofauti, linapokuja suala la maambukizi ya virusi vya ukimwi nani amkamatishe mwenzake?

Huu utandawazi hadi kwenye familia zetu, nani alaumiwe? Binafsi nadhani wajibu ndani ya familia zetu umekosa mwelekeo. Maadili katika usimamizi wa familia zetu yametoweka kabisa. Watu wanaishi ili mradi kumekucha na kila mtu anashika lake bila kutathmini athari zake kimaisha.

Watu wanapeana uhuru wa kufanya mambo bila kuzingatia miiko, miongozo ikiwemo ya kidini na matokeo yake maisha yanaparaganyika pasipo mwelekeo sahihi kwa familia husika.

Mbona mashindano ya aina hii yameleta mauti kwa wengi? Hivi ni vita ambavyo havina mshindi kwani mwisho wa siku wote mtakuwa majeruhi. Hata hivyo, kwa jicho la tatu naona roho ya mitala ikiwatesa wanandoa hao. Ukichunguza familia zao, ipo roho ya kuwa na wake wengi au pia mahusiano na wanaume tofauti? Ni roho inayotesa wengi. Nitajitahidi kuichambua roho hii siku zijazo.

Familia ikifikia hatua hiyo, ujue jahazi linakwenda mrama. Wiki ijayo msomaji wangu nitakuletea kituko kipya eti mke atimkia mjini bila ugomvi, amuacha mume ameduwaa!

**Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Ukiwa tayari kuwa huru kuwasiliana nami kwa kutuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Wanasaikolojia, wataalam afya ya akili, iko wapi ajenda ya kitaifa?

IDADI kubwa ya wanaume hawana mahali pa kupumulia matatizo yao. Mikasa au madhila wanayopitia katika maisha ni mtihani mzito kwao kuung'amua, ukilinganisha na wanawake.

Wanasaikolojia wanasema mwanamke anaongea maneno 24,000 mpaka 26,000 kwa siku. Hii ni kwa sababu yeye anatafuta mara nyingi njia za kuondoa hali ya kihisia anayoisikia ndani yake ambayo inasababisha yeye kuwa na matatizo mbalimbali.

Wakati mwanamke akiona ahueni mapema, unaambiwa mwanamume anazungumza maneno 6,000 mpaka 7,000 kwa saa 24.

Lakini uwezo wa mwanaume kueleza matatizo yake anayopitia ni mdogo sana, ukilinganisha na uwezo wa mwanamke.

Kwa mfano, ukiangalia huu mfumo umetengenezwa pia katika mfumo wa malezi, unaweza kuwa shahidi kwamba namna unavyomlea mtoto wa kiume, ni tofauti na tunavyomlea mtoto wa kike.

Kwamba mtoto wa kiume tunamlea kama ni mtu ambaye ni mlinzi, ni mtu ambaye ni mkakamavu, ambaye hatakiwi kuonekana ananung'unika au kulalamika.

Kwa hiyo, huwa inamnyima mtoto wa kiume kuwa na tabia ya kueleza matatizo aliyo nayo ndiyo maana unaweza ukakuta si tu kuongea, hata kulia mtoto wa kiume, akilia ni tofauti na tunavyomchukulia, tofauti akilia mtoto wa kike.

Ndiyo! Ni kweli wanawake wana marafiki wengi, wana watu wanaowatumia kwenye jamii kueleza matatizo wanayoyapitia, ikiwamo kutafuta msaada. Hiyo kuongea maneno mengi, ni sehemu ya yeye kupumua au kuelezea hisia ambazo ambazo anakuwa anakuwa anapitia katika maisha yake ya kawaida.

Ukienda kwenye nyumba za ibada, mfano kanisani utawakuta wanawake pamoja na kwamba idadi yao ni kubwa, bado kwenye hayo maeneo wanakuwa wengi sana kwa sababu wanatumia njia hiyo kama eneo muhimu la kukabiliana na matatizo wanayopitia kwenye maisha yao ya kawaida.

Ukiangalia wanaume wao, njia zao ni butu kwa sababu wanakimbilia kwenye matumizi ya vilevi kama pombe. Utakuta wamejazana kwenye baa, utakuta wanaangalia mpira na vitu vingine ambavyo ni burudani.

Vitu hivyo kwa wanaume vinasaidia kwa sehemu ndogo sana kulinganisha na maneno ambayo walipaswa kuyazungumza ili kutatua tatizo ndiyo maana tunasema moja ya vitu vinavyochangia sana wanaume kufa mapema ni kushindwa kueleza matatizo waliyo nayo ili kuepukana na msongo wa mawazo.

Wanaume wengi matatizo yao wanayatunza kwenye akili na wanajaribu kupambana nayo wenyewe, kitu ambacho si kizuri.

Watazame wanawake wanayatunza moyoni lakini wao mara nyingi huyatoa kwa marafiki zao, wakiwa wanasogoa mambo yao. Hilo linasaidia kuwapunguzia msongo wa mawazo.

Kwa nini nimeandika leo waraka huu? Nimevutiwa na hoja iliyotolewa mwanzoni mwa wiki hii na Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mkoa wa Tanga, Sharifa Coshuma, wakati akifungua mafunzo ya watalaka na watalakiwa, kujiingiza katika ujasirimali ili kujikwamua kiuchumi.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, aligusia siri ya wanawake wengi, hasa watalaka na watalikiwa, kuishi marefu kuliko wanaume, kwamba ni uvumilifu na kutoishi na vinyongo moyoni.

Kwamba, kuzungumza kwao mambo yao yanayowasibu, kwa kuwa wawazi, ndio tiba sahihi katika jambo lolote.

Ripoti ya 'Tanzania in Figures 2021' iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ya mwaka 2021, inaonyesha wanaume wanaweza kuishi kwa wastani wa miaka 63.7 huku wanawake wakiwa na wastani wa miaka 69, tofauti ya miaka 5.3

Kutokana na ongezeko la matukio yanayoogofya, afya ya akili husababisha wanaume wengi kufa mapema, kwa sababu ya msongo wa mawazo.

Naona, ni vyema sasa, wanasaikolojia na wataalamu wa afya ya akili, wakajitwisha jukumu zito mbele ya la kutoa elimu.

Ni wazi kuwa wakati utofauti wa umri wa kuishi kati ya wanaume na wanawake ukizidi kuongezeka kadiri ya miaka inavyozidi kwenda, tuna kila sababu ya kulibeba sasa suala hili kama ilivyo kwa ajenda ya kupinga ukatili wa kijinsia. Tukutano Jumapili ijayo.


- **Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini.Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com Simu ya mkononi: +255 767 535490**

# HARUSI



Gauni la bi harusi lililobuniwa kwa mwonekano wa ndege aina ya tausi kama linavyoonekana katika picha tofauti. Ni vizuri kuwa tofauti katika siku muhimu kama hiyo

# MITINDO







## FURAHIA 'SWEATPANTS'

# Hustarehesha kwenye mazoezi

MIAKA ya nyuma kujiandaa kufanya mazoezi au kukimbia ilikuwa rahisi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Hali hiyo inatokana na ukweli kwamba hakukuwa na nguo za kufanyia mazoezi, badala yake kila mtu alivaa kivyake bila kujali kama ni sahihi au la.

Lakini ujio wa nguo aina ya sweatpants kwa miaka ya hivi karibuni imefanya suala la mazoezi kuwa moja ya eneo muhimu.

Nguo hizi zinamfanya mtu kuwa na furaha hasa kutokana na upumuaji kuwa rahisi na kustarehesha zaidi.

Kaptura na suruali hizi daima hutoa nafasi ya kuboresha linapokuja suala la mazoezi, haswa kwa upande wa wanaume.

Kaptura na suruali za mazoezi za wanaume zinatakiwa kuwa na hali ya kumfanya mtu mtulivu na mwenye kustarehe bila kujali unatoka jasho kiasi gani.

Nguo za aina hii zimeundwa maalum kwa ajili kunyonya unyevu ili kusaidia kuzuia jasho mbali na kulikausha haraka.

Hii husaidia kuharakisha mchakato wa kupoza na kuweka vizuri zaidi mwili.

UREMBO

Na Mary Geofrey



# HAPA UZEE KWISHA

MAKOVU ya uzee kitaalamu huitwa 'liver spots' au 'sun spots' ambayo huwa doa jekundu au hudhurungi kwenye ngozi ya uso, mikono na shingo.

Katika kesi nyingi, madoa haya huwa yanaongezeka kutokana na miale ya jua.

Pia madoa ya uzee yanaweza kutokea wakati ini likiwa limezidiwa na sumu.

Kwa bahati nzuri, dalili za kwanza za makovu haya ya uzee yanaweza kutibiwa na kutatuliwa kwa urahisi kwa msaada wa tiba rahisi za nyumbani bila hata kwenda hospitali.

Tiba muhimu za nyumbani za kupunguza makovu ya uzee ni kama zifuatazo.

**Siki ya Tufaa**

Ukichukua mchanganyiko wa siki ya tufaa na juisi kitunguu maji kisha ukapakaa kwenye makovu yako utaona maajabu sana.

Asidi ya kitunguu saumu na tufaa husaidia kuyafifisha haya makovu na kukuacha ukiwa na urembo kama ki-jana mdogo.

Hakikisha umechanganya kizibo kimoja cha siki ya tufaa na maji vijiko vitatu kabla ya kutumia.

Unaweza pia kuchanganya siki ya tufaha na maji ya uvuguvugu na kunywa mchanganyiko huu mara moja kila siku, nusu saa kabla ya kula ili kupata ngozi laini na bila makovu ya uzee.

**Juisi ya Aloe Vera**

Juisi ya aloe vera pia inasemekana kuwa yenye ufanisi katika matibabu ya makovu ya uzee.

Wengi wameona matokeo mazuri na ndio maana nakueleza ili uondoe uzee kwenye ngozi yako.

**Matumizi**

Paka kiwango kidogo cha juisi au maji ya aloe vera moja kwa moja kwenye makovu ya uzee kisha fanya masaji kwa dakika 5.

Subiri nusu saa kisha osha uso kwa maji ya uvuguvugu.

Utaanza kuona mabadiliko ya kiasi kikubwa na kuonekana mrembo/mtanashati ndani ya mwezi mmoja.

**Itaendelea...**





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Pika Katles ufurahie maisha

KATLES ni aina ya kitafunwa kinachopikwa kwa kutumia viazi mbatata na nyama ya kusaga.

Hakika ukila katles iliyopikwa kwa ustadi unaotakiwa hutajuta kula chakula hicho.

**Mahitaji**

Nyama ya kusaga kilo moja, viazi mbatata, giligilani, vitunguu swaum, tangawizi, pilipili hoho na ndimu.

Binzari nyembamba, pilipili manga, mayai, unga wa sembe au ngano na mafuta ya kupikia uyapendayo.

**Namna ya kuandaa**

Chemsha nyama yako vizuri na kisha chemsha na viazi hakikisha vinaiva vizuri kabisa.

Katakata hoho, vitunguu maji, karoti katika mfumo ule ule wa vipande vidogo vidogo na ukimaliza hapo chukua mchanganyiko wako wa nyama na viazi uweke katika chombo kimoja.

Chukua vitunguu maji, pilipili hoho, karoti ulivyo katakata weka kwenye mchanganyiko wako wa nyama na viazi, tia kitunguu swaum, kamulia tena ndimu, weka na unga wa binzari nyembamba na pilipili manga, katia na giligilani zako, sasa anza kuchanganya vyote kwa pamoja.

Changanya changanya mpaka utakapo ona vyote vimechanganyika vizuri.

**Namna ya kupika**

Andaa sahani zako za kuwekea madonde yako ya katles zinyunyuzie unga wa sembe ama ngano itategemea wewe wataka unga gani.

Ukishamaliza hapo chukua mchanganyiko wako na utengeneze kwa umbo upendalo kama duara au fimbo.

Baada ya hapo utaviviringisha katika unga wako ulio uchagua wewe na utapanga kwenye sahani, utarudia hivyo katika vidude vyote.

Ukimaliza chukua mayai yako yale manne yavunje na kutia katika chombo huku ukibandika kichomeo chako jikoni na ukishaweka mafuta yako.

Tumia moto wa wastani na mafuta yakishapata moto kiasi cha wewe kuridhika chukua katles zako tia katika mayai zungusha zungusha ili mayai yaingie pande zote alafu weka kwenye kikaangio chako jikoni.

Chakula chako kitakuwa tayari kwa kuliwa wakati wowote na juisi, chai au kinywaji kingine.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# Tengeneza eneo la chakula kulingana na nafasi ya nyumba




ASILIMIA kubwa ya wamiliki wa nyumba hujali sana kuwekeza nguvu zao katika sebule.

Naamini kwamba wengi wanafanya hivyo kwa sababu ndiyo sehemu inayotumika sana katika kuketi wageni na kufanyia mazungumzo mbalimbali.

Pamoja na umuhimu huo, leo nataka tugeukie upande mwingine wa eneo linalotumika kwa chakula (dining room) ambalo pia nalo ni muhimu.

Katika nyumba nyingi, chumba hiki huwa kimetazamana na sebule japokuwa wachache hukitenga na ukuta kinakuwa hakionekani.

Tuanze na kwa hawa ambao chumba hiki kinachotumika kwa chakula kinaonekana.

Hapa nataka tujifunze kwanza ni namna gani tunahitaji kiwe, nini kinapaswa kukaa humo na kitu gani hakipaswi kukaa. Kama hakijakaa vizuri ni namna gani unataka kiwe kulingana na vile unavyo 'design' wewe.

Pia kumbuka kabla ya kuweka kitu chochote, hakikisha unaangalia kwa nafasi iliyopo katika chumba chako hicho.

Baadhi yetu tumezoea kwamba dining lazima kwanza iwe na meza kubwa ama ndefu.

Si lazima uwe na meza ndefu, isipokuwa unachopaswa kuzingatia ni nafasi iliyopo katika chumba hicho na uzingatiaji katika 'desining'.

Ukishajua namna ambavyo unataka kupangilia chumba chako hicho, hapo ndipo unaweza kuamua au kupaka rangi kwa kuzingatia isipishane sana na ile iliyopo sebuleni au iwe katika kundi hilo na hiyo ni kwa chumba cha chakula kinachotazamana na sebuleni.



# Usiweke mshumaa kwenye kisosi



**Na Restuta James**

SHIDA ya umeme inayoendelea nchini na kusababisha mgawo imewafanya watu kutumia mwanga mbadala hasa nyakati za usiku majumbani.

Msomaji mmoja wa ukurasa huu, Diana Kibinga, amenipigia simu na kunieleza adha ya kukatika umeme inavyomchafulia nyumba kutokana na matumizi ya mshumaa.

Anasema ana taa mbili za umeme jua ambazo hazitoshelezi mahitaji ya nyumba yake kwa kuwa ana watoto ambao wakati mwingine wanafanya kazi za shule hadi usiku; jambo linalomlazimisha kuwasha mishumaa.

"Sakafu imechafuka na mishumaa hujapata kuona na wanangu wamevunja visosi naona sasa watakuwa wanawasha na kuiweka chini," anasema.

Inawezekana kuna watu wengine wanashida kama ya Diana na hawajui cha kufanya; hapa nitawashauri.

Ni muhimu sana kuwa na taa ya umeme jua, hata ile ndogo kabisa ili ikusaidie kupata mwanga ndani ya nyumba. Zaidi pia, hii ni salama zaidi kuliko mishumaa kutokana na kwamba inadumu muda mrefu na haihatarishi usalama kama mishumaa.


Hata hivyo, matumizi ya mishumaa hayakwepeki kwa kuwa mbali ya kuleta mwanga, inatumika pia kama pambo ndani ya nyumba. Hii ni kwa sababu, kuna familia zimezoea kuitumia hata kama umeme unakuwepo.

Ili ufurahie mshumaa katika kipindi hiki cha mgawo, hakikisha unajipatia holda zitakazozuia mshumaa kuvuja chini. Kisosi sio rafiki sana kwa kuwa namna ya kuuweka mshumaa ni changamoto.

Jizoeze kutumia mishumaa mikubwa, hii ni rahisi pia kuweka kwenye kisosi kama utakosa holda za kisasa.

Tuwasiliane katika restutajames@gmail.com au 0753333330

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
WE' BABU UNANING'ANG'A-NIA HUOGOPI KUTEKWA?
HAPA NILIPO USHANI-TEKA.
"NGULI" WA RUSHWA
TENGE-NEZENI GARI ACHENI UZEMBE!
NA LIKI-ZIMIKA HASUKU-MI MTU!
HAWAJUI UCHUNGU WA GARI.
WJINGA TU.
GARI LINA-SHITUKA-SHITUKA KAMA LINA DEGEDEGE!
TRAFIKI YUKO WAPI.
MNACHONGA KAMA MNAI-JUA BEI YA GARI!..
LEO NJIA NZIMA NIKI-PISHANA NA MTU LAZIMA AGEUKE!...NNA MVUTO BILA KWENDA KWA MGANGA!
UNAJIDAI UNAISHI USHUWANI MBONA UPO HUKU USWAZI
'NIMEMISI MIGUU YA KUKU NA MAPUPU'
VIJANA BHANA ETI WANATAFUTA 'KUTOBOA' WAKATI NGUO WANAZOVAA ZINA MATOBO!
KWELI "MUME" TUTOKE HUKU TUHAMIE TANDALE?
MAISHA KAMA GWARIDE....! UKISIKIA NYUMAAAAAA GEUKAAAAA!!! UJUE WA MBELE ATAKUWA NYUMA!...
OSTABEI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MVAA NGUO MPYA HAISHI KUJIKAGUA

HABARI KIMATAIFA

# MAELFU WAKIMBIA GAZA KASKAZINI

## -Majeshi ya Israel yaingia kuwasaka Hamas
## -Umoja wa Mataifa yasema hali ni mbaya

MAELFU ya Wapalestina wamekimbilia eneo la kusini mwa Gaza kusaka hifadhi, baada ya Israel kuwataka waondoke ndani ya Saa 24 kabla ya kuanza operesheni ya ardhini kuwasaka wapiganaji wa Hamas.

Kundi la Hamas, linalotambuliwa na Umoja wa Ulaya na Marekani kama la kigaidi, limewataka wakazi wa Gaza kutohama kwenye nyumba zao.

Kwenye misikiti iliyoko ukanda huo limekuwa likiwatangazia watu wasalie majumbani mwao.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu alisema wiki nzima ya mashambulizi ya mabomu ni mwanzo tu wa operesheni katika Ukanda wa Gaza, baada ya zaidi ya watu 1,300 kuuawa kwenye uvamizi wa Hamas ndani ya Israel, Jumamosi iliyopita.

Israel ilidai idadi kubwa ya watu waliouawa, baada ya wapiganaji wa Hamas kuvunja mpaka unaolindwa kwa nguvu kubwa za kijeshi, walikuwa raia wa kawaida.

Ndani ya saa 24 iliyopita, jeshi la Israel lilisema lilifanya msako ndani ya Gaza kujaribu kuwaondosha wale linaowaita magaidi na kugunduwa walipo watu waliotekwa na Hamas.

Hadi sasa, watu zaidi ya 1,900, wengi wao raia na zaidi ya 600 kati yao wakiwa watoto, wameshauawa kwenye wimbi la makombora ya Israel yanayotupwa Gaza, hayo ni kwa mujibu wa wizara ya afya ya Palestina.

Jeshi la Israel lilisema Hamas iliwachukuwa mateka 150, wakiwamo raia wa Israel, wageni na wale wenye uraia wa nchi mbili na kwenda nao upande wa Gaza.

Hata hivyo, Hamas walisema siku ya Ijumaa kwamba watu 13 kati ya mateka hao wameuawa kutokana na mashambulizi ya anga ya Israel yanayoendelea.

Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Ujerumani, Annalena Bearbock, ambaye aliitembelea Israel juzi, alisema Hamas inawatumia wakazi wa Gaza kama ngao.



Baadhi ya Wapalestina wakiondoka upande wa kaskazini mwa Gaza kuelekea kusini ya ukanda huo baada ya Israel kuwapa Saa 24 kuhama. **PICHA: ALLIANCE**

### HALI MBAYA GAZA

Israel imechukua hatua ya kuukatia Ukanda wa Gaza huduma zote muhimu, ikiwamo maji, mafuta, umeme na chakula.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres ameilezea hali kwenye Ukanda huo kwamba imefika kiwango cha hatari kubwa, na ametowa wito wa Umoja huo kupatiwa fursa ya kuingia kusambaza misaada ya kibinadamu.

Rais Joe Biden wa Marekani, ambaye nchi yake unaiunga mkono Israel, alisema hali ya kibinadamu ni muhimu kupewa kipaumbele.

Hali ya wasiwasi imezuka Mashariki ya Kati kote na maeneo mengine, huku waandamanaji wenye hasira wakijitokeza mitaani kuwaunga mkono Wapalestina, katika nchi za Lebanon, Iraq, Iran, Jordan na Bahrain.

Waziri Mkuu wa Mamlaka ya Palestina, Mohammad Shtayyeh, ameituhumu Israel kwa kuendeleza "mauaji ya kimbari kwenye eneo la Ukanda wa Gaza.

Hata hivyo, msemaji wa Netanyahu, Tal Heinrich, ameliambia shirika la habari la AFP kwamba kinachotokea Gaza ni matokeo ya makosa ya Hamas.

### MAJENGO YAANGUSHWA

Zaidi ya majengo 1,300 katika Ukanda wa Gaza yameharibiwa wakati wa mashambulizi yanayoelekea kudumu kwa muda wa wiki moja.

Kulingana na Shirika la Umoja wa Mataifa la kutoa misaada ya kibinadamu (OCHA) lilisema nyumba 5,540 ziliharibiwa na karibu nyumba 3,750 zaidi ziliharibiwa vibaya na haziwezi kukaliwa.

Jeshi la Ulinzi la Israel jana asubuhi limekanusha taarifa zinazosema kuwa huenda lilipata miili ya baadhi ya mateka wakati wa msako mkali uliofanyika huko Gaza.

Msemaji Luteni Kanali Richard Hecht, alisema "Madai haya si sahihi.Hatuna habari kuhusu suala hilo," .

### RUSSIA YAINGIA RASMI

Russia ilisema naibu waziri wake wa mambo ya nje anatarajia kukutana na wawakilishi wa Hamas nchini Qatar wiki ijayo kujadili kuachiliwa kwa mateka wa Israel.

Shirika la habari linalomilikiwa na serikali ya Russia la Ria-Novosti lilisema nchi hiyo imejitokeza kama nchi inayoweza kuleta amani kutokana na kuwa na uhusiano mzuri kati ya Hamas na Iran.

Nchini Uingereza, umati wa watu umekusanyika nje ya jengo la Shirika la Utangazaji (BBC) katikati mwa jiji la London wakiandamana kuwaunga mkono Palestina.

Maandamano hayo ambayo yalielekea Whitehall ambako ni makao makuu ya serikali yanajumuisha watu wa rika zote na familia kadhaa zenye watoto.

Kundi moja lilipeperusha bendera kubwa ya Palestina huku waandamanaji wakiimba, "Palestine huru, huru - kuikalia kimabavu ni uhalifu".

### MATAIFA YAPINGA KUHAMA

Mataifa ya Qatar na Saudi Arabia yamepinga hatua ya kuhamishwa watu kwa nguvu ndani ya Gaza, baada ya Israeli kutoa saa 24 Wapalestina wanaoishi Gaza kaskazini kuelekea kusini.

Taarifa kutoka wizara ya mambo ya nje ya Qatar ilisema inataka kuondolewa kwa mzingiro wa Ukanda wa Gaza, na kutoa ulinzi kamili kwa raia wa Palestina kulingana na sheria za kimataifa na za kibinadamu.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Saudi Arabia, pia imeandika kupitia mtandao wa x watu wasihamishwe kwa nguvu na kuruhusiwa kwa mahitaji muhimu kuingia Gaza.

"Kwa sababu kuwanyima mahitaji haya ya kimsingi ili kuishi kwa utu ni sawa na ukiukaji wa sheria za kimataifa za kibinadamu".

### WANAOHAMA WASHAMBULIWA

Ripoti zilizotoka juzi jioni kuwa msafara wa magari yanayoelekea kusini mwa Gaza yameshambuliwa kwa mabomu.

Video zinazoonyesha watu wakiwa wameuawa katika eneo la tukio.

BBC imethibitisha shambulio hilo lililotokea katika mtaa wa Salah-al-Din ni moja ya njia mbili za uokoaji zilizokubaliwa kutoka kaskazini mwa Gaza kuelekea kusini.

Barabara hiyo ilijaa msongamano wa magari siku nzima jana huku wakazi wa Gaza walioko kaskazini wakizingatia onyo la Israel la kutaka kuondoka eneo hilo.

Takriban maiti 12 zilionekana kwenye picha, wengi wao wakiwa wanawake na watoto.

Mpangilio wa vivuli kwenye video unapendekeza kuwa ilirekodiwa karibu 11:30 jioni.

Wizara ya Afya ya Palestina ilisema watu 70 waliuawa katika eneo hilo, na ililaumu Israel kwa shambulio hilo.

Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) lilisema linachunguza tukio hilo, lakini likaeleza maadui wake wanajaribu kuzuia raia kuondoka kaskazini.

MAKALA

# MFUMO WETU WA ELIMU HUJENGA UBWANA



Na Magabilo Masambu

**Mazingira hayo humfanya mtoto huyo kuanza kujiona yu mtu anayefaa kufanyiwa kazi, badala ya yeye kufanya kazi kwa bidii ili kuwasaidia wazazi kutafuta pesa za masomo yake shuleni.**

WAZAZI wengi na jamii kwa jumla humtazama mtoto ambaye yuko shuleni kwa jicho la mtoto asiyefaa kufanya kazi fulani fulani katika jamii. Jamii na wazazi wengi huwaona watoto wao waliosoma na wanaosoma kama vijiungu watu. Watani zangu Wahaya wanawaita wote hao "Ishomile" lakini shule yao haikuwasaidia. Tujiulize Je, ni wanafunzi wetu wangapi hudiriki kutumia siku zao za mapumziko kufanya kazi ambazo zitainua hali ya maisha ya watu katika jamii bila malipo?

Mfano, mtoto anayetokea katika familia maskini ambayo pengine shughuli yao kubwa ni kilimo, arudipo likizo kutoka shuleni huwa hafanyi tena shughuli za shamba, tofauti na mwanzo kabla hajaenda shuleni.

Kibaya zaidi ni kwamba hata pesa ya kumsomeshea inatokana na kilimo hicho cha wazazi wake, lakini anaporudi kutoka shuleni wakati wa likizo mtoto huyo huheshimiwa na kuogopwa kiasi cha kumwona hafai tena kwenda shambani kwa kuwa sasa amekuwa msomi.

Mazingira hayo humfanya mtoto huyo kuanza kujiona yu mtu anayefaa kufanyiwa kazi, badala ya yeye kufanya kazi kwa bidii ili kuwasaidia wazazi kutafuta pesa za masomo yake shuleni. Tabia hii ya kumwona mtu aliyesoma ni tofauti sana na watu wengine ambao hawakwenda shule na kumuona anastahili huduma za upendeleo tofauti na wengine katika jamii, ndiyo inayowafanya wasomi wengi kutumia nafasi zao kujitofautisha na kujipa nafasi ya kipaumbele kuliko wananchi wanaowachagua.

Kijana aliyezoea kufanya kazi katika jamii yake, bila kujali kiwango chake cha elimu huwa ni rahisi kuwa mzalendo, kwasababu shughuli wanazofanya wanajamii kwa kiasi kikubwa, huziona za kawaida hivyo huzifanya bila wasiwasi. Kama jamii tunapaswa kuwafundisha vijana wetu kazi za jamii zetu bila kujali elimu zao.

Mkulima aliyekaa kijijini kwa miaka 20 akilima pamba au tumbaku, atakuwa na elimu kubwa zaidi katika mazao yake hayo kuliko bwana shamba mwenye shahada katika fani ya kilimo. Je, kama hatupendi kujifunza kutoka katika jamii zetu kwa kuwa tumesoma sana ni kweli tutapata maprofesa watakaoweza kulisaidia taifa?

Suala la maadili kwa wanafunzi na watoto wetu limekuwa shida sana. Hili nalo linatokana na kitendo cha kuwaabudu sana watoto wetu kwa sababu ya elimu zao. Leo hii ni wazazi wachache sana wanaoweza kuwaadhibu watoto wao walioko ngazi ya sekondari, kisa? Eti hawa ni wasomi ukiwaadhibu utawachanganya katika masomo yao! Waafrika tusikubali kuimbishwa nyimbo zenye tamaduni za mataifa mengine, sisi tunayo saikolojia na tiba zetu vilevile.

Katika nchi zetu za kiafrika, malezi ya saikolojia huchukua nafasi ndogo sana, maana maisha yetu bado si ya kuchagua. Bado tumo katika jitihada za kupambana na umaskini, kwa hiyo tusidanganywe kuwa saikolojia inatakiwa kufanya hivi na vile na kwamba kiboko ni kibaya sana kwa mtoto!

Mtoto mjinga weka fimbo. Hata mfalme Sulemani anasema: "Ujinga umefungwa ndani ya moyo wa mtoto, lakini fimbo ya adhabu itaufukuzia mbali (Mithali 22:15) na kwamba usimnyime mtoto wako mapigo, maana ukimpiga kwa fimbo hatakufa, bali utamwokoa nafsi yake na kuzimu." (Mithali 23:13-14).

Waafrika tusiige yasiyokuwa yetu, tuna yetu mazuri sana kama wao wanawapa watoto wao uhuru wa kumshitaki baba na mama mahakamani ni wao. Malezi ya watoto kwavyovyote vile lazima yatofautiane kwa sababu ya kutofautiana kimazingira, lakini tunayo miiko na tamaduni zetu nzuri sana.

Kitendo cha wazazi kutowaadhibu watoto wao majumbani, huwafanya watoto wajione wanaonewa wanapoadhibiwa na walimu wao shuleni. Tumewahi kusikia mara nyingi, mwanafunzi akisema "Mama aliyenizaa hajawahi kuniadhibu mwalimu ataniadhibuje?" Ebo!

Wakati mwingine wazazi husikika pia wakisema: "Ole wake mwalimu atakayemwadhibu mwanangu, atakutana na mkono wa sheria." Ukiwa na tabia ya kuwalinda watoto wako dhidi ya maovu, kuna siku utatumia gharama kubwa sana kuajili wanasheria ili wawatetee mahakamani dhidi ya maovu makubwa zaidi.

Kulea watoto kama kuku wa kisasa haifa kwani huwafanya watoto wawe wajinga na tegemezi nyakati zote hata wakiwa watu wazima. Watoto wa aina hiyo huwa ni mizigo mizito isiyobebeka, wakati wazazi wao wanapofariki na kuwaachia watu wengine kuwalea.

Umekufa lakini unawaachia ndugu zako mizigo isiyobebeka, badala yake wanabaki kulaumu kwamba baba yetu au mama yetu angelikuwapo, tusingelipata mateso haya tatizo kumbe ni kwa sababu ya malezi mabovu uliowapatia wakati ukiwa hai. Lea watoto wako katika misingi am-

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Nimevuka maji ya shingo mgongo haukuloa



Na Adam Fungamwango

**Ni tofauti na sasa kijana anaweza kuamka asubuhi, akaoga, akajiremba na kupaka pafyumu, akavaa nguo nzuri, halafu akaenda kukaa sehemu kama vile saluni au duka wanalouza nguo kutwa nzima anapiga stori.**

MKUU! Baba! Ile methali ya kikwetu isemayo milima haikutani lakini wanadamu hukutana, ni ya kweli kabisa na yenye busara.

Tazama! Tarishi alikuja toka Natal, akalia, 'Makumazahn amekufa! Nchi haitamwona Makumazahn tena.' Haya yalitokea zamani sana.

Na sasa, tazama hapa katika nchi ngeni ya harufu mbaya namwona tena Makumazahn, rafiki yangu.

Ndiye bila shaka. Manyoya ya mzee mbweha yameingia mvi, lakini macho yake na meno yake ni makali kama zamani."

Haya maneno yanatoka kwenye kitabu chenye simulizi kali isiyosahaulika kiitwacho 'Mambo ya ajabu yaliyompata Allan Quatermain na wenzake.'

Kiliandikwa na mwandishi mmoja aitwaye H. Rider Haggard zamani sana, lakini nakala ya kwanza kwa lugha ya kiswahili ilitolewa mwaka 1968.

Ni kitabu maarufu sana kwa vijana wa Kitanzania wa miaka ya 1970, 1980, kabla ya kupigwa marufuku kwa kipindi fulani, lakini kwa sasa vimerudi tena.

Ni moja kati ya vitabu vya kibabe, majigambo, vita, vinavyojenga kujiamini. Nadhani hata kupigwa kwake marufuku ilikuwa kwa sababu hiyo. Vijana waliovisoma kwa wakati huo walileta uhalisia hata kwenye maisha ya kawaida.

"Mara ile alinitambua akawa ananiamkia.' Mkuu, mkuu wa zamani. Mkuu, mkuu! Baba! Makumazahn, mzee mwindaji, muuaji wa tembo, mla simba, mwerevu akeshaye! Hodari, mwepesi! Ambaye risasi zake kabisa hazikosi shabaha, apigaye shabaha ya kweli, rafiki mwaminifu.

Haa haaa...ni wewe uliyekuwa tayari kukutana uso kwa uso na Umsolopagaaz,wa damu ya chaka mshindi wa wasioshindika, tazama maombi yako yametimia.

Umsolopagaaz alimshushia yule mjivuni shoka moja, pigo takatifu likaachanisha shingo na kiwiliwili mjivuni akaanguka chini na kufa papo hapo.

Akaingalia maiti ya adui yake na kusema hakika, lilikuwa pigo zuri.

Kutabu hivi na vingine vingi viliondolewa na kutopatikana tena, au kwa kiswahili kizuri kupigwa marufuku kwa madai ilikuwa inaharibu maadili ya vijana.

Hata hivyo, ukiangalia sana unagundua vijana wa zamani hawakuharibiwa na vitabu hivyo, ila ilikuwa ndiyo hulka yao.

Wengi, hasa wa kiume walikuwa wababe, wajivuni, wenye nguvu, wanaopenda zaidi kazi za kutumia nguvu kuliko zile laini wakidai ndiyo za kiume na ili wakuhesabu mwenzao kuwa ni kijana uliyekamilika ni lazima kwanza uwe umeshawahi kuwapiga hata watu wawili au watatu mbele ya macho yao, kufanya kazi ngumu na kutokuwa na mambo mengi yasiyo ya lazima kwa mwanaume kama kupaka mafuta, kuvaa nguo nzuri na mpya kila kukicha, au kukaa tu kutwa nzima bila kufanya shughuli yoyote.

Ni tofauti na sasa kijana anaweza kuamka asubuhi, akaoga, akajiremba na kupaka pafyumu, akavaa nguo nzuri, halafu akaenda kukaa sehemu kama vile saluni au duka wanalouza nguo kutwa nzima anapiga stori.

Kijana wa aina hii zamani hakuwa na sifa ya kukaa na vijana wenzake. Watamwita tu 'mtoto wa mama.'

Tabia hiyo, ukiongea na aina ya vitabu vya kibabe ya aina hiyo, vilizidi kuwafanya wawe wakakamavu na wenye utayari.

Hata bendi ya OTTU Jazz ilichukua baadhi ya maneno kutoka kwenye kitabu hicho na kutengeneza wimbo waliouita 'Chuma Kikoli Moto.'

Uliimbwa na wanamuziki wengi lakini kwa asilimia kubwa Athumani Momba ndiye aliyeupamba sana na unaweza ukasema ndiye mtunzi.

Wimbo huo ulitungwa na Suleiman Mwanyiro, mpiga besi maarufu kuwahi kutokea nchini.

Walichomoa maneno kutoka kwenye kitabu hicho na kutunga wimbo huo wenye maneno yafuatayo.

"Usinichezee yaya, usichezee chuma cha moto, usinichezee yaya, usichezee chuma cha moto.

Washindwa waganga na waganguzi, sembuse wewe mwana mkiwa, jiepushe na masikitikito, nimetoka Bara na Nyika.

Usinichezee yaya, usichezee chuma cha moto, usinichezee yaya, usichezee chuma cha moto.

Washindwa waganga na waganguzi, sembuse wewe mwana mkiwa, jiepushe na masikitikito, nimetoka Bara na Nyika

Yeye yeye Dadi, chuma kikoli moto yeye yeye Dadi, mpela ya belemwene.

Usilete ujuaji unaumia bure, nimevuka maji ya shingo, mgongo haukuloa, wewe bwana mdogo umeipata hiyo hooo, bwana mdogo utaumia bure

Yeye yeye Dadi, chuma kikoli moto yeye yeye Dadi, 'mpela ya belemwene.'

Usilete ujuaji unaumia bure, nimevuka maji ya shingo, mgongo haukuloa, wewe bwana mdogo umeipata hiyo hooo, bwana mdogo, utauawa bore.

Yeye yeye Dadi, chuma kikoli moto yeye yeye Dadi, mpela ya belemwene."

Uliimbwa kiswahili na kuongezwa kidogo maneno kwa lugha ya Kingoni. Hivi ndivyo vitabu vya enzi hizo na hizi ndizo nyimbo zake zilizowajengea vijana kuwa wakakamavu badala ya mapenzi kila kukicha.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Kafie kwenu-15

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James. Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

USIMPENDE na kumyeyekea tajiri tu kwa sababu ya kutarajia kupata kitu kutoka kwake, fanya hivyo hata kwa watu duni, masikini na fukara kama wewe. Hawa huwa hawana pesa, lakini watakuombea baraka, dua na kukuongoza njia pia." Ni usia wa mwisho wa Farida kwa kijana wake.

Wiki mbili tu baadaye alifariki dunia na kumuacha kijana wake akiishi kwenye chumba kimoja cha uani alichokuwa amepanga Vingunguti.

Kodi ilipoisha James alishindwa kulipia na kuamua kuondoka. Akarudi kulala kwa rafiki zake kama alivyokuwa akifanya hivyo wakati mama yake yupo hai.

Alipoanza kufanya kazi zake za vibarua, vingi alivipata akiwa Magomeni na Kinondoni. Ndipo alipoamua kupanga kwenye nyumba moja duni, Kinondoni Moscow.

Siku moja James aliamua kufuata ramani aliyompa marehemu mama yake mpaka akafika nyumbani kwa aliyedaiwa ni baba yake kwa mujibu wa marehemu mama yake Farida, mzee Joel Kamagi.

Aliwakuta watoto wa mzee huyo ambao tayari walikuwa wameshakuwa wakubwa na wamerithi mali ya baba yao.

Alijitambulisha kwa jina, na akasema kama alivyoambiwa na mama yake.

Watoto wa mzee huyo hawakubisha, lakini wakamwambia hana chake pale kwa sababu yeye ni mtoto wa nje ya ndoa.

Na wao wakamueleza madhila aliyopata mama yao mzazi Monica pindi alipogundua mzee ametembea na binti wa kazi.

Mkubwa wao, Alfonce ndiye aliyempasha kuwa hawangeweza kumsaidia chochote kwa sababu kwanza mama yake Farida ndiye aliyesababisha vifo vya wazazi wao kwani baada ya tukio lile familia ile haikuwa na amani tena.

"Wala si uongo na mama yako hakukudanganya. Ila yeye ndiye aliyesababisha mama yetu kupata ugonjwa wa moyo na ukamuweka kitandani kwa zaidi ya miezi sita akafariki dunia.

Na hii ni baada ya mama yako kukiri kuwa ujauzito alionao ulikuwa wa baba. Pamoja na mzee kutaka kukataa lakini ushahidi woteulionyesha hivyo na akakiri, akaomba msamaha.


Pamoja na hayo mama hakuwa kwenye hali nzuri, ugonjwa wa moyo ukamtafuna hadi akafariki. Kifo chake nacho kilisababisha baba kukosa amani, akawa mtu anayeweweseka hivi mara kwa mara, mwaka mmoja baadaye akafariki dunia." Yalikuwa ni maneno ya Alfonce akimwambia James.

"Baada ya kifo cha baba tulikaa na ndugu wa pande zote mbili na kukubaliana kwa mujibu wa utamaduni na kabila letu, hakuna mtoto yeyote wa nje ya ndoa atakayekuja au kuletwa ili adai sehemu ya mali ya marehemu."Akapigilia nyundo.

James ambaye alikaa kimya muda wote akiwaangalia kwa zamu ndugu zake wanaume wawili na mwanamke mmoja ambao ni wakubwa kwa umri kwake kwani tukio lile lilipokuwa linatokea wao walikuwa wanaingia hatua ya ujana na bado walikuwa wanasoma. Alfonce alipomaliza naye akatamka.

"Nashukuru sana, ila hata kama sitapata hata kipande cha sabuni cha urithi kutoka kwa mzee, lakini nilichofurahi ni kuhakikishiwa kuwa baba yangu ni mzee Joel Kamagi. Nilichokuwa nahitaji kumfahamu tu baba yangu kama alivyonisimulia mama, na leo kwa mara ya kwanza nimemuona kwenye picha ile pale mliyotundika ukutani. Nimewaona pia na nyinyi ndugu zangu. Najua mimi sijafanya kosa lolote. Kosa lilifanywa na wazazi wangu. Baba yangu mzee Kamagi alitembea na mama yangu Farida miaka mingi nyuma wakati akifanya kazi za ndani hapa wakati ana mkewe wa ndoa Monica. Mama akafukuzwa. Leo hii mimi naishi kwa tabu mitaani. Na nyinyi ndugu zangu mnanikata. Mnaniambia mimi ni mtoto wa nje ya ndoa. Sawa nimekubali, naondoka kuendelea na maisha yangu mtaani. Kuweni na amani, wala msidhani kama nitarudi tena hapa, ila Mungu akipenda tutaonana." Akamaliza James kwa sauti ya simanzi lakini ya kujiamini.

Akanyanyuka, akaibusu picha ya baba yake akaondoka huku watoto wa mzee Kamagi wakimuangalia kama mtu ambaye amechanganyikiwa. Wakatazamana, wakatabasamu.




**Mkubwa wao, Alfonce ndiye aliyempasha kuwa hawangeweza kumsaidia chochote kwa sababu kwanza mama yake Farida ndiye aliyesababisha vifo vya wazazi wao kwani baada ya tukio lile familia ile haikuwa na amani tena.**

****************************************

Upepo mkali uliochanganyikana na hali ya baridi uliashiria mabadiliko ya hali ya hewa, tofauti na ilivyokuwa mchana.

Kulikuwa na jua kali lililowalazimu wakazi wa jiji la Dar es Salaam waliokuwa ndani na maofisini kutupia virekebisha hewa, feni na AC, wengine wakijipoza na juisi pamoja na maji baridi.

Lakini hali ilibadilika ghafla juu. Mawingu fulani hivi yalitanda na kibaridi kikaingia, baadaye ikafuatiwa na upepo mkali.

Ilikuwa ni majira ya saa 11 jioni hivi. Gari aina ya Toyota Fielder lilipaki maeneo fulani hivi jijini Dar es Salaam. Ndani akateremka kijana mmoja mrefu mwembamba aliyekuwa amevaa jinsi ya bluu iliyoiva.

Alivaa fulana nyeusi iliyokuwa na maandishi kadhaa meupe. shingoni alijipamba na cheni kadhaa zilizokaa vema na kumpendezesha.

Chini alivaa raba yenye kitambaa cheusi, lakini ikibeba soli nene nyeupe. Kichwani alivaa kofia iliyo aina ya 'cape' na mawani ya jua.

Kijana huyo aliyekuwa akiendesha gari alionekana alikuwa peke yake, alifunga mlango na kuangaza huku na huko.

Alionekana kushangaa mandhari ya eneo analoliona. Na kila kitu alichokiona alionekana kukishangaa au kukifurahia.

Alianza kutembea kwa hatua za taratibu, akiwa ameshika funguo mkononi huku akiuchezeshachezesha.

Alionekana kutembea taratibu, lakini kwa uhakika. Japo kwenye macho ya baadhi ya watu alionekana mgeni, lakini mwenyewe hakujali. Alitembea na kushuka taratibu na ilionekana kama mtu anayefayamu njia za uchochoroni ingawa ni mgeni, hadi sehemu moja hivi ambayo alisimama.

Aliiangalia kwa makini kama vile anaiangalia kwa mara ya kwanza. Akatikisa kichwa. Ni kama vile alikuwa akijaribu kukumbuka alichokiona. Alisimama kwa zaidi ya dakika 10. Baadhi ya watu walipita hapo na kumuona amesimama.

Kila mmoja aliyemuona alikuwa na wazo moja tu kichwani mwake. Ni mnunuzi wa nyumba kutokana na eneo hilo alilokuwa amesimama na kushangaashangaa.

Kwa mbali alionekana msichana mmoja mdogo akitokea maeneo ya chini zaidi kuelekea pale alipokuwa jamaa mpya mgeni aliyekuja maeneo yale.


Kwa namna ambayo haikufahamika mara moja, ilionekana kama kila mmoja alikuwa akimtazama mwenzake.

Yule jamaa alionekana kumtazama msichana anayekuja na yeye pia alimtazama kwa makini sana.

Alipofika karibu, mgeni akavua mawani na kofia. Hakujulikana nia yake ni kutaka atambulike au vipi! Msichana akazidi kumtazama na kumshangaa. Hakuna aliyemsemesha mwenzake. Baada ya sekunde 30 hivi msichana bila kuongea neno lolote, aligeuka na kurudi mbio kurejea alikotoka.

Jamaa alitabasamu, akarudisha miwani na kofia yake kila kimoja mahala pake na kuanza taratibu kurudi alikopaki gari lake.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# SHUSHO, MULIRO KUPAMBA IMBA TOGETHER 2023

Tamasha la Imba Together litafanyika tena mwezi Oktoba katika miji ya Winston Salem na North Carolina nchini Marekani.

Katika jukwaa la tamasha hilo litakalofanyika kwa siku mbili kuanzia Oktoba 27, litapambwa na waimbaji maarufu wa Injili kutoka Tanzania Christina Shusho na Gloria Muliro wa Kenya.

Tamasha la Imba Together linaandaliwa na Anna J Simtaji tangu mwaka 2017.

Akizungumza na BT, Simtaji muandaaji wa Imba Together, amesema tamasha hilo litawaongezea waimbaji wanawake uwezo wao kisanaa na kumjua Mungu kupitia mafunzo.

# Poshy Queen maokoto kwake hatari

MPAMBAJI wa video za muziki, Poshy Queen amesema amechoshwa na baadhi ya wanaume ambao wanadhani yeye ni muhuni na anatumia umbo lake vibaya.

Poshy Queen amesema licha ya mwenyezi Mungu kumpatia umbo linalovutia, lakini hawezi kumkubalia kila mtu anayemtamani na badala yake anazingatia uwezo wake wa kipesa.

"Namshukuru Mungu kunipa umbo kama hili, lakini sitaki wanaume wenye tamaa, nataka wanipe pesa ndio kila kitu, hivyo kama hujanipa hela hakuna mapenzi," alisema Poshy.




# Ziiki yajivunia mafanikio ya wasanii

KAMPUNI ya usambazaji na ukusanyaji mapato kwa wasanii wa muziki duniani Ziiki, imesema kwa kushirikiana na serikali itaendelea kuhakikisha kila msanii wanayemsimamia analipwa mapato yake kulingana na kazi anayoifanya.

Akizungumza hivi karibuni Meneja wa kampuni hiyo kwa Afrika Mashariki na Kati, Camilla Owora, amesema utaratibu huo unafanyika ili kuhakikisha kila msanii waliyeingia naye mkataba ananufaika na kazi zake.

Amesema kila kinachofanywa katika kazi ya kusambaza na kusimamia mapato yanatokana na makubaliano, hivyo hakuna msanii anayepunjwa au kukosa mapato yake kutokana na mauzo yanayofanyika katika majukwaa ya muziki duniani.

"Kila tunachokifanya kipo ndani ya mikataba yetu na wasanii na serikali kupitia Basata inajua na ndio maana malalamiko yanakuwa machache hasa kutokana na wasanii ambao kwa namna moja wanakataa kusaini malipo yetu. Tunajitahidi kuelimisha kuhusu utaratibu wa ukusanyaji mapato na usambazaji wa kazi zao wengi wanakubaliana nasi," amesema Camilla.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAGUIRE ATAKIWA JANUARI

WEST Ham inafikiria ofa mpya kwa ajili ya kupata huduma za mlinzi wa England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 30, dirisha la Januari iwapo ataendelea kukosa muda wa kucheza pale Manchester United (***ESPN***)

### GUEHI ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inamfuatilia mlinzi wa Crystal Palace na Timu ya Taifa ya England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 23, kabla ya kuhama msimu ujao. (***Mail)***

### BARCA YAMTAKA MITOMA

BARCELONA inavutiwa na winga wa Brighton na Timu ya Taifa ya Japan, Kaoru Mitoma mwenye umri wa miaka 26. (***Mundo Deportivo)***

### MARTIAL RUKSA KUONDOKA

MANCHESTER United ipo tayari kumruhusu mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 27 kuondoka katika klabu hiyo Januari. (***Football Insider)***

### LINGARD ATUA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa zamani wa Nottingham Forest, Jesse Lingard (30), ambaye mara ya mwisho alichezea England mwaka 2021, anakaribia kusajiliwa na Al Ettifaq ya Saudia, lakini hawezi kucheza mechi yake ya kwanza hadi Januari kutokana na sheria ya wachezaji wa kigeni nchini humo. (***Sky Sports***)

### SUDAKOV AKARIBIA JUVE

KLABU ya Juventus inaongoza mbio za kuwania saini ya kiungo wa Shakhtar Donetsk na Ukraine, Georgiy Sudakov mwenye umri wa miaka 21, huku Arsenal , Manchester City na Brighton pia zikimwindwa. (***TEAMtalk)***

### MIRANDA KUTUA MILAN

AC Milan inataka kumleta beki wa kushoto wa Real Betis na Hispania, Juan Miranda mwenye umri wa miaka 23 kama msaidizi wa Theo Hernandez. (Sky Sports Italia)

### EBERL ATAJWA LIVERPOOL

LIVERPOOL imeonyesha nia ya kumfanya Mjerumani, Max Eberl kuwa Mkurugenzi wa Michezo wa timu yao. Eberl huyo mwenye umri wa miaka 50, ambaye pia anasakwa na Bayern Munich, hivi majuzi aliacha nafasi hiyo katika klabu ya RB Leipzig (***Bild)***

### BELLINGHAM NYOTA GHALI

KIUNGO wa kati wa Real Madrid na England, Jude Bellingham (20), ndiye mchezaji wa pamoja wa thamani zaidi katika LaLiga kwa mujibu wa data mpya. Thamani yake ni pauni milioni 130 inamfanya kuwa sawa na mchezaji mwenzake wa Real, Vinicius Jr ***(Transfermarkt)***

### CHIPUKIZI BRAZIL WAGOMBEWA

MANCHESTER City, Chelsea, Arsenal na Manchester United zote zinataka wachezaji wawili wa Palmeiras, ambao ni raia wa Brazil, Estevao mwenye miaka 16 na Luis Guilherme (17), wanaocheza nafasi ya mshambuliaji na kiungo. (***90min)***

### CLEMENT AITEGA RANGER

PHILIPPE Clement anataka mkataba wa miaka minne iwapo atakuwa kocha wa Ranger, huku klabu ya Saudia Al-Shabab pia ikimtaka Mbelgiji huyo. (***Record***)

## DONDOO Z... A
## MAGAZETI Y...



# UFARANSA, UBELGIJI, ZAFUZU EURO 2024

## Ronaldo pia aipeleka Ureno huku akifikisha mabao 125...

**AMSTERDAM,** Uholanzi

KYLIAN Mbappé na Cristiano Ronaldo wote walifunga mabao mawili kila mmoja na kusaidia Ufaransa na Ureno kupata nafasi ya kufuzu kushiriki Fainali za Mataifa ya Ulaya (Euro 2024).

Ubelgiji pia imefuzu kushiriki michuano hiyo itakayofanyika nchini Ujerumani.

**Vigogo hao watatu wa Ulaya walihitaji ushindi ili kufuzu kwa michuano hiyo na washambuliaji wao nyota walihakikisha wanapata nafasi hiyo muhimu.**

Mabao mawili ya Mbappé yalisaidia kupata ushindi wa 2-1 dhidi ya Uholanzi huko Amsterdam ikiwa ni ushindi wa sita kwenye Kundi B.

Mbappé alianza kufunga dakika ya saba alipomshinda Lutsharel Geertruida kwa krosi kutoka upande wa kulia iliyopigwa na Jonathan Clauss na kumpita kipa wa Brighton, Bert Verbruggen, ambaye alikuwa akiichezea Uholanzi kwa mara ya kwanza.

Lilikuwa ni goli la 41 la Mbappé la kimataifa, likimvuta sawa na nguli wa Ufaransa Michel Platini.

"Mimi si mtu wa kuwa na wasiwasi, na hasa si kuhusu Kylian," Kocha Timu ya Taifa ya Ufaransa, Didier Descamps alisema.

"Alionyesha leo (juzi), hakuna cha kuwa na wasiwasi. Anapokuwa hivi ni wazi Ufaransa wana nafasi zaidi za kushinda."

Mbappé alifunga bao la pili dakika ya 53 walipoona vizuri na Adrien Rabiot kwenye ukingo wa eneo la hatari la Uholanzi kabla ya kuachia kombora dhidi ya Verbruggen.

Kiungo wa kati wa Feyenoord, Quilindschy Hartman, katika mechi yake ya kwanza kamili ya kimataifa, aliifanya timu hiyo kumaliza na ushindi wa mabao 2-1 zikiwa zimesalia dakika 10 kumalizika. Lilikuwa bao la kwanza Ufaransa kufungwa kwenye kampeni hiyo.

Ugiriki ilipanda hadi nafasi ya pili ikiwa na alama 12 baada ya Giakoumakis na Giorgos Masouras kufunga bao moja kila mmoja nana kuifunga Ireland 2-0 huko Dublin.

Mabao mawili ya Ronaldo yaliboresha rekodi yake ya mabao ya kimataifa hadi 125 katika mechi 202 na kupelekea Ureno kushinda 3-2 dhidi ya Slovakia.

Ronaldo alifunga kwa penalti dakika ya 29, na kumpelekea kipa wa Slovakia Martin Dúbravka njia mbaya na kabla ya kuongeza bao la pili.

Mshambuliaji, Goncalo Ramos alikuwa amewapatia wenyeji Ureno bao la kuongoza kwa kichwa dakika 11.Baada ya David Hancko kurudisha bao moja kwa Slovakia katika kipindi cha pili, Ronaldo alirudisha faida ya mabao mawili kwa krosi ndogo kutoka kwa Bruno Fernandes iliyomkuta kwenye lango la mbali.

"Cristiano yuko katika hali nzuri, anacheza dakika nyingi na kufunga mabao mengi akiwa na klabu yake," alisema Kocha wa Ureno, Roberto Martinez baada ya mchezo huo.

"Kwenye timu ya taifa ana uzoefu mkubwa, ni kichocheo na rejea kwa vijana. Sote tunafanya kadri tuwezavyo, sio mchezo wa mtu binafsi, ni mchezo wa pamoja."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI

NORWAY
VERSUS
SPAIN

1 | 3.91
X | 3.38
2 | 1.97

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MAGUIRE KUTETA NA MABOSI WA UNITED

**MANCHESTER,** England

HARRY Maguire amekiri wanapaswa kukaa na mabosi wa Manchester United kuzungumza kama ataendelea kucheza mara moja katika timu hiyo.

Mlinzi huyo wa kati wa kimataifa wa England amepata mashaka na kukosa nafasi ya kutosha ya kucheza kwenye kikosi cha Mashetani Wekundu kiasi cha kumfanya avuliwe kitambaa cha unahodha.

Maguire, mwenye umri wa miaka 30 alihusishwa kujiunga na West Ham wakati wa majira ya joto, lakini mpango huo haukukamilika na kusalia kwenye kikosi cha Manchester United akidhamiria kumshawishi kocha wa timu hiyo, Erik ten Hag kumpatia nafasi ya kucheza.

Huku fainali za Mataifa ya Ulaya 'Euro 2024' zikikaribia, Maguire amesema kukosa nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha Manchester United kunaweza kuhatarisha nafasi ya kuitwa katika Timu ya Taifa ya England.

Kocha Mkuu wa England, Gareth Southgate amekuwa shabiki mkubwa wa beki huyo wa kati pamoja na kupita kwenye wakati mgumu katika maisha yake ya soka kwa sasa.

# *KMKM SC yachapwa Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAMBO yamezidi kuwa magumu kwa mabingwa watetezi, KMKM SC baada ya kukubali kufungwa na Malindi bao 1-0 katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi jioni.

Bao peke katika mechi hiyo lilipachikwa na Omar Ame dakika ya 46 baada ya kuunganisha mpira wa adhabu uliotinga wavuni moja kwa moja na kuifanya KMKM ipoteze mechi ya pili mfululizo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu alisema walicheza vizuri dakika zote lakini walishindwa kupata bao kutokana na mchezo huo kuwa makali kwa pande zote.

Msimu alisema hata goli lilofungwa lilitokana na mpira wa adhabu ambapo walinzi wa KMKM walipoteza umakini katika kuzuia na kuwapa faida wapinzani wao.

"Tulicheza kwa kujilinda na umakini kwa dakika zote, lakini kosa moja ndio lilotuadhibu hadi kupelekea kufungwa, siku zote michezo migumu kama hii timu itakayopata bao basi lazima watalinda bao lao," Msimu alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Malindi, Sheha Khamis alisema licha ya kupata ushindi lakini anawapongeza wapinzani wao KMKM kwa kucheza vizuri katika dakika zote za mchezo huo.

"Tumepata ushindi, tumefurahi kwa sababu lengo letu lilikuwa alama tatu, lakini bado kikosi chetu kinahitaji kujijenga zaidi ili tuzidi kuwa timu bora kadri tunaposhuka dimbani,"alisema kocha huyo.

CHEZA USHINDE KASINO

# MAVUNDE AFUNGUKA GGML IKIWAPA BASI GEITA GOLD

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde amewataka wadau wa soka mkoani hapa kuinga mkono Geita Gold FC ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara badala ya kuuachia mgodi wa GGML peke yake, imeelezwa.

Mavunde ametoa rai hiyo katika hafla ya kukabidhi basi la kisasa lenye viti 45 lililotolewa na GGML kwa ajili kuisafirisha Geita Gold FC kuelekea katika mechi zake mbalimbali.

"Mgodi wa GGML leo (jana), mmeandika historia kubwa, kitendo mlichofanya cha kutoa gari la usafiri kwa timu kitaongeza morali, kuendesha timu ni kazi kubwa zipo baadhi ya timu hapa nchini zinashiriki Ligi Kuu lakini hazina usafiri kabisa, GGML endeleni kuifadhili timu hii kwa sababu inawatangaza pia," alisema Mavunde .

Waziri huyo pia amewataka wadau wengine kujitokeza kusaidia ujenzi wa uwanja kukamilika kwa wakati ili mechi zote za timu hiyo zifanyike mkoani humo na kuacha kupeleka michezo ya Simba na Yanga mkoani Mwanza.

Kiongozi huyo ametoa muda wa miezi sita ili kukamilisha ujenzi huo wa uwanja ambao utakuwa ni faraja kwa mashabiki wa soka wa mkoani hapa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong alisema kwa miaka mingi mgodi huo umekuwa fahari katika kuisaidia jamii na kuongeza ushirikiano wao na timu ya Geita Gold ni mfano .

"Tumekabidhi basi la kisasa kwa timu ya Geita Gold FC ikiwa ni kuiunga mkono timu hiyo, si kitendo cha wema bali inaonyesha ahadi yetu ya kudumu kwa maendeleo na ustawi, pia tumejitolea kukuza vipaji kwa vijana wetu," alisema Terry .

"Tunaipenda timu yetu ya Geita Gold FC, mtambue mnapofanya vibaya wadau wa soka Geita wanaumia," Mbunge wa Geita Mjini, Constantine Kanyasu alisema.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (mwenye jezi ya bluu), akiashiria kukabidhi basi kwa uongozi wa Geita Gold FC ambalo limetolewa na GGML kwa ajili ya usafiri wa timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu. Wengine ni viongozi wa GGML, Geita Gold na Chama cha Soka cha Mkoa wa Geita (GEREFA). **PICHA: ALPHONCE KABILONDO**

# *Yanga kusajili watatu wapya*

INATOKA UK. 24

nye mazoezi," alisema meneja huyo.

Simba imeifunga Al Ahly mara zote inapokutana nayo hapa nchini, tatizo linakuwa inapokwenda ugenini nchini Misri.

Mwaka 1984, Simba iliifunga Al Ahly mabao 2-1, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza ikiwa ni Kombe la Washindi Barani Afrika (sasa Kombe la Shirikisho), kwa mabao ya Zamoyoni Mogella 'Golden Boy' na Mtemi Ramadhani, lakini ikapoteza kwa magoli 2-0 ilipokwenda Cairo na kutolewa kwa jumla ya mabao 3-2. Zilikutana tena mwaka 2019 katika wa kwenye hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ikipigika nchini Misri mabao 5-0, lakini ikashinda nyumbani bao 1-0, shukrani Meddie Kagere na mwaka 2021 Simba iliichapa tena Al Ahly hapa nyumbani bao 1-0 kupitia Luis Miquissone katika mechi ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini ikafungwa tena ugenini goli 1-0.


SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 15/10/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2111 | Fuenlabrada vs Gimnastic Tarragona | 2.70 | 2.96 | 2.55 |
| 13:00 | 5455 | UD Ibiza Eivissa vs Recreativo Huelva | 1.52 | 3.73 | 5.72 |
| 14:00 | 2909 | Umeaa FC vs Motala Aif | 1.82 | 3.62 | 3.52 |
| 14:30 | 5489 | SSV Ulm vs Dynamo Dresden | 3.22 | 3.33 | 2.13 |
| 15:00 | 1802 | Burgos vs Villarreal B | 1.98 | 3.26 | 3.61 |
| 15:00 | 2451 | Virtus Entella vs Gubbio | 1.82 | 3.40 | 4.40 |
| 15:00 | 2948 | Benevento vs AZ Picerno | 2.06 | 3.24 | 3.61 |
| 15:00 | 3193 | TSV Havelse vs Meppen | 2.06 | 3.62 | 2.96 |
| 15:00 | 5377 | Juve Stabia vs Catania | 2.81 | 3.07 | 2.57 |
| 15:30 | 5918 | Willem II Tilburg vs Den Bosch | 1.43 | 4.40 | 5.93 |
| 16:00 | 3336 | Falkenbergs vs FC Trollhattan | 1.73 | 3.54 | 4.00 |
| 16:00 | 4167 | NK Ilirija vs ND Beltinci | 5.20 | 3.80 | 1.50 |
| 16:00 | 4379 | Georgia vs Cyprus | 1.37 | 4.64 | 8.65 |
| 16:00 | 5118 | NK Nafta vs Triglav | 1.88 | 3.54 | 3.39 |
| 16:00 | 5562 | Arsenal W vs Aston Villa Lfc W | 1.31 | 4.78 | 7.73 |
| 17:00 | 1109 | Cray Wanderers vs AFC Hornchurch | 3.71 | 3.71 | 1.78 |
| 17:00 | 5429 | Wexford Youths vs Cobh Ramblers | 2.23 | 3.33 | 2.77 |
| 17:15 | 1807 | Latina vs Monopoli | 2.01 | 3.18 | 3.86 |
| 17:15 | 2793 | Recanatese vs Arezzo | 3.40 | 3.24 | 2.14 |
| 17:15 | 3009 | Barcelona B vs CD Teruel | 1.72 | 3.25 | 4.30 |
| 17:15 | 3784 | Vicenza vs Renate | 1.67 | 3.62 | 5.14 |
| 17:15 | 4052 | FC Andorra vs Alcorcon | 2.06 | 3.02 | 3.66 |
| 17:15 | 4222 | Taranto Sport vs Crotone | 2.73 | 3.04 | 2.67 |
| 17:15 | 4493 | CD Eldense vs Elche | 3.21 | 3.11 | 2.19 |
| 17:30 | 4333 | Preussen Munster vs 1860 Munich | 2.19 | 3.52 | 2.95 |
| 17:45 | 5451 | Cambuur vs NAC Breda | 1.90 | 3.62 | 3.42 |
| 18:00 | 4421 | Krka vs Brinje Grosuplje | 2.15 | 3.43 | 2.83 |
| 18:30 | 3066 | Liverpool W vs Everton W | 1.79 | 3.46 | 3.97 |
| 18:30 | 3457 | Rangers vs Cobreloa | 5.49 | 3.76 | 1.53 |
| 19:00 | 1429 | Zamora CF vs Pontevedra | 2.18 | 3.12 | 3.02 |
| 19:00 | 1468 | Ponferradina vs Deportivo La Coruna | 2.75 | 3.01 | 2.48 |
| 19:00 | 2189 | Switzerland vs Belarus | 1.13 | 7.62 | 22.21 |
| 19:00 | 4857 | Czech Republic vs Faroe Islands | 1.12 | 8.03 | 23.25 |
| 19:00 | 5414 | Lugo vs SD Logrones | 1.90 | 3.16 | 3.87 |
| 19:30 | 1166 | Leganes vs Amorebieta | 1.96 | 3.06 | 3.95 |
| 19:30 | 3522 | Atletico Madrid W vs Barcelona W | 15.31 | 6.94 | 1.12 |
| 19:30 | 4191 | Eibar vs Huesca | 1.52 | 3.63 | 6.36 |
| 19:30 | 5914 | Spal vs Fermana FC | 1.55 | 3.93 | 5.87 |
| 21:00 | 3018 | Real Sociedad B vs Leonesa | 2.31 | 2.95 | 3.05 |
| 21:15 | 3308 | River Plate (URU) vs CA Boston River | 2.36 | 3.07 | 2.77 |
| 21:30 | 1328 | Atletico Rafaela vs Chacarita Juniors | 3.43 | 3.19 | 2.02 |
| 21:30 | 1945 | Quilmes vs Racing De Cordoba | 1.86 | 3.24 | 3.92 |
| 21:30 | 2064 | Brown Adrogue vs CA Atlanta | 1.72 | 3.33 | 4.61 |
| 21:45 | 3738 | Poland vs Moldova | 1.24 | 5.72 | 12.72 |
| 21:45 | 5206 | Ponte Preta vs Atletico GO | 2.84 | 2.89 | 2.49 |
| 21:45 | 5501 | Wales vs Croatia | 3.76 | 3.34 | 2.02 |
| 21:45 | 5748 | Romania vs Andorra | 1.14 | 7.41 | 20.10 |
| 21:45 | 5784 | Norway vs Spain | 3.91 | 3.38 | 1.97 |
| 21:45 | 5983 | Turkey vs Latvia | 1.18 | 6.79 | 15.90 |
| 23:00 | 2863 | Club Atletico Palmaflor vs Jorge Wilstermann | 3.00 | 3.56 | 2.06 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Oktoba 15, 2023

Nipashe





## Maguire kuteta na United

UKURASA 22




Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Maxi Nzengeli (kushoto), akijaribu kumtoka mchezaji mwenzake wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa kuivaa Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Oktoba 25, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

## Stars, Sudan kazini

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kuvaana na wenzao wa Sudan katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa leo katika mji wa Jeddah, nchini Saudi Arabia.

Ni mchezo maalumu unaotambulika katika kalenda ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), na inatarajiwa kuwa sehemu ya maandalizi ya kikosi cha Kocha Mkuu, Adel Amrouche kuelekea Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), zitakazofanyika mapema mwakani.

Akizungumza na gazeti hili jana, mshambuliaji wa Taifa Stars, Simon Msuva, amesema wachezaji wa timu hiyo wanaahidi kuendelea kupambana katika kila mechi iliyoko mbele yao.

Msuva alisema motisha wanayopata kutoka kwa Rais, Samia Suluhu Hassan inawaongezea nguvu ya kupambana ili kufanya vizuri zaidi na wanaipenda.

"Tunaomba wazidi kutuombea, tumevuka hatua moja na kwenda hatua nyingine, tuna mchezo mwingine dhidi ya Sudan, tutafanya vizuri, hatutamwangusha," alisema Msuva.

Naye Novatus Miroshi alisema anafuraha kuendelea kuitwa katika kikosi hicho na kwake anaamini watajiimarisha kuendelea kupeperusha vyema bendera ya Tanzania.

"Ni mchezo muhimu kwa sababu utatuweka nafasi nzuri katika viwango vya FIFA, pia kila mchezaji anataka kujituma ili kujitafutia nafasi ya kuitwa katika kikosi kitakachokwenda AFCON," alisema Novatus.

Naye Ofisa Habari wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo aliliambia gazeti hili kikosi kiko vizuri na kinachosubiriwa ni kipenga kwa ajili ya mechi hiyo ambayo itawaongezea pointi katika viwango endapo watashinda.

Amrouche ameita nyota 28 wanaocheza ndani na nje ya Tanzania kwa ajili ya mechi hiyo ya kirafiki.

# Yanga kusajili watatu wapya

## ●●● Gamondi atema cheche, Simba yawaota Al Ahly...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

IKIWA imetinga hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga inajipanga kusajili wachezaji wapya watatu katika usajili wa dirisha dogo kwa lengo ya kuhakikisha wanafanya vyema zaidi katika michuano hiyo ya kimataifa, imefahamika.

**Yanga imedhamiria kuimarisha kikosi chake kwa sababu wanaamini itawasaidia kufanya vizuri katika vita ya kutetea taji la Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na taji la Kombe la FA ambayo wanayashikilia.**

Dirisha dogo la usajili litafunguliwa rasmi na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ifikapo Desemba.

Habari zilizopatikana kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema huenda uamuzi wa kusajili wachezaji hao wapya umetolewa na Kocha Mkuu, Miguel Gamondi ambaye anataka kuona kila idara inakuwa imara na hatimaye wanafikia malengo.

Chanzo hicho kiliendelea kusema Gamondi anahitaji kupata straika mpya mmoja na nafasi nyingine mbili zitakazobainika zinahitaji kuongezewa nguvu.

Taarifa zaidi ziliendelea Gamondi amehitaji kuongeza nguvu baada ya kubaini ndani ya kikosi chake kuna aina tatu ya wachezaji.

"Kocha amesema kwa sasa kuna wachezaji wanaojituma kweli kweli na kuifanya Yanga, pili kuna wachezaji wazuri lakini wanategea mazoezi na tatu ni wale ambao amedai hawastahili kuwamo na kuichezea timu kubwa kama Yanga," kilisema chanzo chetu.

Kiongozi huyo alisema kwa sababu hiyo, Gamondi anadaiwa kutaka kuondoa wachezaji ambao hawana faida na timu na anaamini wapya watakaosajiliwa watashirikiana na wenzao waliopo ili kuipambania timu hiyo.

"Unajua kikosi kwa sasa kimebaki na baadhi ya wachezaji tu, wengine wamekwenda kuzitumikia nchi zao kwenye timu za taifa kwa hiyo waliobaki amekuwa wakiwaangalia kwa ukaribu zaidi, nafasi hii inamsaidia kuwajua wachezaji ambao mpaka sasa bado hawajaonyesha kitu chochote au kumshawishi," chanzo chetu kiliongeza.

Hata hivyo, chanzo chetu kilisema kabla ya Gamondi kukamilisha zoezi la kutaja majina ya wachezaji asiowahitaji, ametoa mechi nne kwa baadhi ya wachezaji ili kukamilisha mchakato wake.

"Kocha anasema anataka wachezaji walio tayari kuipambania Yanga na kuifikishia malengo yake, ameshakaa na wachezaji ambao wanaona hawatimizi wajibu wao na kuzungumza nao, kipindi cha dirisha dogo huenda akapendekeza tukasajili straika mmoja na wachezaji wengine wawili kwenye nafasi nyingine tofauti," aliongeza mtoa habari wetu.

Wakati huo huo, uongozi wa Simba umesema kikosi chao kinaendelea vyema na mazoezi na wanaamini malengo yao ya kuweka historia msimu huu katika michuano ya kimataifa wanayoshiriki yatatimia.

"Hata Al Ahly wanaifahamu Simba na hawataona kitu kipya tukiwafunga hapa nyumbani kwa sababu tuliwahi kufanya hivyo, safari hii tumejipanga kutaka kuwatoa kwenye mashindano hayo kwa kuwafunga hapa na kwao kwenye mchezo wa marudiano," alisema Ahmed Ally, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba.

Aliongeza benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Roberto Oliveira 'Robertinho' limeendelea kukisuka kikosi chao na ametamba tayari ameanza kutengeneza 'dawa' ya kuwaondoa Al Ahly katika mashindano hayo.

"Kikosi kipo kambini kwa wachezaji ambao hawako katika majukumu ya timu za taifa, wale majeruhi tayari wanaendelea vizuri akiwamo beki yetu, Henock Inonga ambaye ameitwa katika kikosi cha DRC, Manula (Aishi) amerejea vizuri kwe-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >